**Mbivu**, mbichi hukumu mke wa Bilionea Msuya kujulikana leo
UKURASA 4



**Manufaa** ya ziara za Rais nje yaanikwa
UKURASA 5

**Askofu** matatani madai ya kuwazuia waumini kushiriki sensa na chanjo
UKURASA 7



**VAN DIJK: TUPO KATIKA NJIA SAHIHI**
UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Februari 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581595

www.ippmedia.com

www.twiter.com/nipashetz
Maoni@guardian.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US
The Guardian digital


## Mataragio gumzo uteuzi, utenguzi vigogo UK. 4

UHABA WA SUKARI

# Hatimaye serikali yakunjua makucha



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe

•**Sheria** kufumuliwa, kibano chaja wenye viwanda ... *Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### SEKTA BINAFSI KUSHIRIKISHWA UWEKEZAJI WA BAGAMOYO SEZ

SERIKALI imesema itaishirikisha kwa karibu sekta binafsi katika kutekeleza mradi wa Kanda Maalumu ya Kiuchumi ya Bagamoyo (SEZ)...



### Familia watu 16 yasimulia ilivyolizwa na mganga feki

UKURASA 3

## Matumaini yarejea uhakika umeme UK. 2

**MICHEZO** SIMBA: TUTAWAFURAHISHA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Matumaini makubwa umeme yarejea

**Na Christina Mwakangale**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, amewatoa hofu Watanzania kuhusu hali tete ya upatikanaji wa umeme ambayo imedumu kwa miezi kadhaa.

Mhandisi Mramba amesema mgawo wa umeme unatarajiwa kumalizika wakati wowote baada ya kuwapo kwa uhakika wa maji katika baadhi ya vyanzo vya nishati hiyo.

Mramba aliyasema hayo jana, Ikulu, Dar es Salaam kwamba hali hiyo inatokana na mitambo miwili kuwa katika hatua za mwisho za majaribio kabla ya kuanza kuzalisha megawati 470.

"Unaweza ukaamka kesho au keshokutwa ukakuta mgawo hamna. Tuko mwishoni kabisa, muda wowote umeme utaingia.

Wataalamu wako kwenye hatua za mwisho wataingiza megawati 235."

"Mfumo wa umeme umegawanyika katika sehemu kuu tatu; kwanza katika kuzalisha umeme; kusafirisha umeme na kufanya usambazaji umeme kwenda kwa mtumiaji.

"Uzalishaji hutegemea zaidi mitambo ya kufua umeme na kwa Tanzania, inatumia gesi asilia, maji na katika gridi ya taifa uko mdogo ulioko Nyakato unaozalisha megawati 30, ukitumia mafuta. Nchini tegemeo kubwa la nishati ni katika maji na gesi asilia. Mitambo yake imeunganishwa pamoja na kupewa jina la gridi," alisema.

Kuhusu mfumo wa usafirishaji unaotumika, alisema uko wa nguzo kubwa za chuma, zikiwamo zinazotoka Kidatu hadi Dar es Salaam au Kihansi - Dar es Salaam. Kwamba umeme huo ni mwingi na haupokewi na watumiaji wa kawaida.

Sehemu ya tatu ya mfumo wa umeme, anasema ni usambazaji, ambao hutumia nguzo za kawaida kwenye miji, kwenye transfoma na vituo vidogo vya usambazaji, mfumo unaotumiwa zaidi mijini.

**TATIZO LILIPO**

Mramba alisema tatizo kubwa la umeme limeegemea katika sehemu mbili ambazo ni uzalishaji na usambazaji na kwamba changamoto kubwa ni katika usafirishaji.

"Uzalishaji usipokidhi mahitaji ndipo tunakuwa na upungufu wa umeme unaosababisha mgawo kwa sababu umeme uliopo hautoshi mahitaji ya watu wote, hivyo unalazimika kuugawa, hawa uwape kwa muda huu na hawa muda huu.

"Usambazaji na mahitaji havioani, mahitaji ni makubwa kuliko umeme unaozalishwa. Kwenye usambazaji kule ndiko kuna miundombinu ukiwapo umeme wa kutosha na miundombinu ina changamoto, bado umeme unaweza kukatika.

"Sasa ukikatika kutokana na miundombinu, unakuwa sio mgao, kwa sababu kuna nguzo imedondoka, transfoma imepata hitilafu, hayo yataendelea kuwapo na kufanyiwa kazi kila siku," alisema Mramba.

Mramba alisema Bwawa la Mwalimu Nyerere linatarajia kupunguza uhaba wa umeme kwa kuwa upo katika hatua za mwisho.

"Tuko katika hatua za mwisho kabisa, mwisho kabisa. Kwa sababu tuna mitambo miwili ambayo tunatarajia itakamilika katika muda mfupi sana ujao.

"Mtambo wa mwanzo umeshafanyiwa majaribio yote na kufaulu. Kilichobaki ni kuingiza umeme katika gridi ya taifa. Mahitaji ya umeme tuliyo nayo nchini ni kati ya Megawati 300 hadi 500.

Kwa mfano leo (jana) asubuhi, tulikuwa na mahitaji ya Megawati 304 kwa hiyo, ukipata 235 utaona kiasi gani unapunguza upungufu zaidi ya asilimia 80," alifafanua.

Mramba alisema mtambo wa pili pia umeshafanyiwa majaribio bila kutumia maji, kuangalia kama vifaa viko sawa na yamefaulu na sasa jaribio linalofuata ni mitambo kuzungushwa wa kutumia maji.

"Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa lina maji mengi na mwaka huu ni mwaka wa maajabu, kwa wiki tatu zilizopita maji yanayoingia katika bwawa imevunja rekodi.

Bwawa la Mtera ni mita za ujazo takribani 1,000 kwa sekunde, haijawahi kutokea.

Maji mengi yaliyoingia yametokea Dodoma na Singida, si Mto Ruaha mkuu ambao ni tegemeo.

"Tumebakiza mita tano tu, Bwawa la Nyerere kujaa, wakati awali tulitarajia kutumia misimu miwili," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na mgeni wake Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta wakati alipowasili Ikulu Tunguu Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

# Serikali yakunjua makucha uhaba sukari

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI inakusudia kupeleka mabadiliko ya sheria inayosimamia soko la sukari nchini ili kuondoa usambazaji kwa kundi moja huku ikiwanyoshea kidole baadhi ya wenye viwanda kushindwa kuingiza kiwango kinachotakiwa na kupandisha bei holela. Hivyo kuwaumiza watumiaji.

Pia amewaonya wenye viwanda waliopewa vibali kuingiza bidhaa hiyo kutoka nje lakini hawajafanya hivyo huku kukiwa na mfumo wa usambazaji unaolazimisha mwananchi kubeba mzigo wa gharama.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza jana Ikulu, Dar es Salaam alisema kwa sasa kuna upungufu wa sukari ambao utamalizika hivi karibuni kutokana na hatua zinazochukuliwa.

Katika kikao hicho kilichoandaliwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Bashe alisema hadi sasa wafanyabiashara 84 wamekamatwa kwa tuhuma za kuficha sukari na watafikishwa mahakamani hivi karibuni.

Bashe alisema sukari inazalishwa na mkulima mdogo na mkubwa ambao hupeleka kiwandani kuzalisha na kwamba tasnia hiyo imekuwa himilivu kwa miaka miwili na kwamba tatizo linalojitokeza sasa lilianza mwaka 2017/18.

Alisema mwaka huu zaidi ya tani 300,000 zitaingizwa kutoka nje na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) itaendelea kuingiza bidhaa hiyo. Alisema uamuzi huo umefikiwa kwa sababu suala la sukari ni kwa ajili ya usalama wa nchi na hadi mwezi ujao, zitaingizwa tani 60,000 na hali itazidi kutengamaa.

"Tuna changamoto kubwa ya wafanyabiashara kufanya uhuni. Tumeshakamatwa 84 na tuko kwenye hatua za mwisho kuwapeleka mahakamani. Haiwezekani mtu ananunua sukari Sh. 2,500 hadi 2,800 na Kwenda kuuza Sh. 4,000 hadi 4,500 wakati kuna bei elekezi. "Tutaendelea na operesheni ya kukamata hadi bei itakaporudi kwenye njia sahihi. Haiwezekani mfano Kagera Sugar ana msambazaji mmoja yuko Mwanza anahudumia mikoa 11. Serikali haiwezi kuruhusu, tumewalinda vya kutosha lakini kwa uwezo wa Mungu mwezi wa sita kwenye bunge la bajeti nitapeleka mabadiliko ya sheria kwa ajili ya kuruhusu biashara huru ya sukari. Watashindana kama wengine wa kutoka nje watapata vivutio," alisema.

Waziri Bashe alisema viwanda vilipewa vibali vya kuingiza tani 10,000 ili kufikisha 50,000 lakini viwanda viwili kati ya vinne vimeingiza tani 2,000 kila kimoja vingine vikiwa havijaagiza na kwamba Kiwanda cha Bagamoyo pekee ndicho kinaingiza tani zote kwa mujibu wa kibali.

"Tumewaambiwa wenye viwanda hata wao tutawachukulia hatua kwa sababu wana wajibu kuwasimamia mawakala wao," alisema.

Waziri Bashe alisema kama serikali isingechukua hatua ya NFRA kuingilia nchi ingekuwa kwenye tatizo zadi na kwamba soko la sukari limekuwa likilindwa na inapotokea tatizo, wafanyabiashara wanatengeneza mazingira ya kuficha ili bei ipande.

"Msingi wa bei ya sokoni kuongezeka ulianzia kiwandani Desemba, mwaka jana. Walipandisha kwa Sh. 650 na muuzaji wa rejareja akaongeza kwa Sh. 850. Hawa wote (kiwanda na wakala) waliongeza Sh. 1,400," alisema.

Kuhusu hali ya upatikanaji wa sukari nchini, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengesi, alisema mahitaji ya sukari ya kawaida (brown sugar) ni tani 552,000 ya viwanda ni tani 255,000 na kwa sasa hali ya uzalishaji ni tani 445,000 na kuna upungufu wa tani 200,000.

Alisema hadi juzi, uzalishaji ulikuwa tani 352,018 sawa na asilimia 79 ya lengo na kwamba kiasi kilichoko sokoni ni tani 8,116 na tani 4,449 zilizotoka nje ya nchi, huku mwenendo wa bei ukiwa Sh. 4,500.

**KAULI WENYE VIWANDA**

Wakizungumza na Nipashe, wenye viwanda ambao hawakutaka kutajwa majina yao huku wakionyesha vibali, walisema walipewa vibali vya kuagiza sukari Januari, mwaka huu, na Bodi ya Sukari ambavyo mwisho wake ni Juni, mwaka huu, na kwamba wameshaagiza kwenye masoko mbalimbali duniani.

Ofisa Utawala wa Kiwanda cha Sukari cha TPC, Jaffari Ally, alisema walipokea kibali Januari 8, mwaka huu kwa matumizi ya nyumbani ambacho kina muda wa miezi sita kuanzia Januari 5 hadi Juni 30,mwaka huu na wanaruhusiwa kutumia mipaka ya Dar es Salaam, Tunduma, Tunduma, Kasumulu, Mwanza, Bukoba na Mtukula.

MITCHELL DRILLING TANZANIA LIMITED

Cheti cha usajili namba 97193
Sheria ya makampuni, 2002
(KIFUNGU 334 (1))

MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha Mitchell Drilling Tanzania Limited (kampuni), yenye usajili namba 97193, kilichofanyika tarehe 20 Desemba 2023 mazimio maalumu yafuatayo yalipitishwa:

1. Kufuatana na kifungu 331 (1) (b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. Wanahisa wamemteua Joseph Lyimo wa Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

JOSEPH LYIMO
MFILISI wa Mitchell Drilling Tanzania Limited

# Familia yafunguka walivyoibiwa na mganga feki

**Na Maulid Mmbaga**

FAMILIA ya watu 16 inayodai kunyeshwa kitu kinachodhaniwa kuwa sumu na mtu aliyejifanya mganga wa kienyeji, imefunguka mengi yaliyojificha.

Tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita na kutolewa taarifa na Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, baada ya familia hiyo, yenye makazi Vijibweni, Kigamboni mkoani Dar es Salaam kukutwa mahututi.

Mwandishi wa habari hii alifika eneo la tukio na kuzungumza na dada mkubwa wa familia, Zenna Harisi, ambaye alisimulia chanzo cha tukio hilo na kubainisha kuwa chanzo cha kukutana na mtu huyo ni mdogo wake ambaye anauza uji, aliyekwenda naye kama mteja.

Alisema baada ya kumuuzia (uji) wakati akiwa anakunywa, ndipo alipomwambia kuwa ana dawa ya kuponya matatizo mbalimbali.

Zenna alisema baada ya mganga huyo kueleza hivyo ndipo mdogo wake akamwambia kuwa mama yake anasumbuliwa na miguu huko nyumbani. Alisema wawili hao walibadilishana namba na ndipo siku ya Jumapili alipokwenda nyumbani kwao.

"Alivyokuja alituuliza kuwa tuko tayari kwa ajili ya yeye kumshughulikia mama yetu tukasema ndiyo, akasema familia yote tukusanyike akawa anatengeneza dawa zake, kwanza akampa baba na wadogo zangu wa kiume na kike waende wakaoge.

"Baada ya hapo akasema mama anatatizo kwa hiyo lazima amtoe hicho kitu, akafanya kama mazingara fulani anayoyajua yeye, akatufunika na shuka, tukaona kuna kitu kakiangusha kama hirizi.

Mara akasema hapo nje kuna kitu, akatuambia tutoke akamwambia mdogo wangu, 'fukua hapo' akatia maji, kikatoka kitu," alisema.

Anaongeza: "Akaturudisha tena ndani akahesabu kama tulivyo pale akaomba gazeti kila mtu akachana kipande chake. Akachanganya dawa zake akatulambisha wote. "Alivyomaliza hapo akasema, wadogo zangu wawili anaona ndio wanamatatizo sana, bi mkubwa (akimaanisha mama) ameshamalizana naye ana afadhali."

Zenna alisema wakati huo, dada yake alikuwa kama anagalagala chini na huyo mganga akadai kuwa mdudu ndo anamtoka. Alisema wakati akiendelea kufanya vitu vyake na wao dawa ikawa anazidi kuwalevya.

"Akatuuliza vyumba vyetu vilipo na kututaka twende tukalale. Alitupa bakuli ambayo imewekwa yai akasema, kila mtu akae chumbani kwake na akiwa anaangalia yai hilo kuna kitu tutakiona," alisimulia Zenna.

Alisema kabla hajaingia chumbani aliambiwa akawaamshe watoto ambao pia, walilambishwa dawa na kuwaambia nao wakalale.

Alisema aliwachukua wazazi wao na kuwapeleka chumbani kwao na kuwaambia waendelee kuangalia mayai hayo na kila mtu ataona kitu kikitokea.

"Baada ya muda alikuja chumbani kwangu na kuniuliza kuwa, alimuona binti yangu ameshika simu kubwa iko wapi? Nikamwambia simu yake ninayo, kwani vipi? Akasema anataka kuipakaa dawa pia, lakini alivyotoka nikaichukua nikaidumbukiza kwenye tenga la nguo chafu.

"Aliporudi mara ya pili nilimuona kama mwenye mshangao, akaniuliza yaani wewe hadi sasa hivi hujalala? Nikamwambia nitalala vipi wakati umeniambia niangalie yai ndio nitaona matokeo nikilala itakuwaje?" alimhoji.

Alisema baada ya kumweleza hivyo, huyo mganga akamwambia asiwe na shida na kumtaka asinzie na majibu yatapatikana.

"Baada ya muda alianza kusinzia.

Kumbe wakati huo mtu huyo alikuwa ameshaingia kwenye vyumba vingine na kuzima taa huku akipekuwa na kuiba fedha. Wakati huo wazazi na familia nzima tulikuwa hatujielewi," alisimulia.

Ilipofika saa 10:00 usiku, alisema alishtuka usingizini na alipokwenda kuwaamsha watoto ili wajiandae kwenda shuleni, kila aliyemwamsha hakuamka zaidi ya kugalagala kitandani na baadhi kutapika.

Baada ya tukio hilo alikwenda kwa majirani kuwaeleza na ndipo wakapata msaada wa kupelekwa hospitalini.

"Wakati huo yule mtu alikuwa ameshaondoka. Baba aliibiwa Sh. 450,000, dada Sh. 107,000 pamoja na simu sita kubwa tatu na ndogo nne. Hadi sasa watoto bado hawako sawa na hawajaanza kwenda shule," alisema.

**BABA AFUNGUKA**

Baba wa familia hiyo, Harisi Amani, alisema tangu alipopatiwa dawa hizo amepatwa na tatizo la miguu kama mke wake na kushindwa kuendelea na shughuli zake za kila siku. Alisema siku ya tukio alipewa dawa na kunawa uso na baada ya hapo akapata kizunguzungu.

"Nilipopelekwa chumbani nilimuona akiingia (chumbani) mara mbili na kila alipokuja alikuwa anatulazimisha tulale. Kama alirudi tena nilikuwa nimeshapoteza fahamu. "Sikujua nini kiliendelea hadi fahamu iliponirudia nikajikuta niko hospitali ya Wilaya Kigamboni saa 7 mchana, shughuli zangu ni za baharini, lakini hadi sasa sina nguvu ya kufanya kitu chochote, hata chakula majirani ndio wanaotusaidia," alisimulia Amani.

Amani alisema licha ya mtu huyo kuwafanyia kitendo hicho, amekuwa akituma ujumbe mfupi wa maandishi kwa ndugu ukitaka watume fedha akidai mzee yupo hospitalini anaumwa huku baadhi wakituma.

Katika taarifa yake, Kamanda Muliro alisema mtuhumiwa huyo bado anatafutwa na kuwataka wananchi kuwa makini na wimbi la matapeli wanaojifanya waganga wa kienyeji na kuishia kuiba.

Kamanda Muliro alitaka jamii kuwaficha watu wanaowahisi kuwa wanajihusisha na aina hiyo ya utapeli ili wachukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.


TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
TACOBA
"Our Bank for Our Development"

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

**YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Kumi wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank Plc** utafanyika siku ya Jumanne tarehe **19 Machi, 2024**, katika **Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU, Tandahimba** kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00) asubuhi** kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita.**
   Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 24/06/2023
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.**
   Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 24/06/2023
5. **Kujadili na kupokea Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2023.**
   **5.1** Taarifa ya Wakurugenzi wenye Dhamana ya Uongozi.
   **5.2** Taarifa ya Meneja Mkuu.
   **5.3** Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Disemba 2023.
6. **Azimio Maalum la kuhamisha Mali na Madeni ya Tandahimba Community Bank Plc Kwenda Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
7. **Azimio Maalum la kuidhinisha kubadili jina la Tandahimba Community Bank Plc kuwa Tandahimba Community Plc.**
8. **Azimio Maalum la kuidhinisha kufungwa kwa kampuni ya Tandahimba Community Plc baada ya kuhamisha mali na madeni kwenda Tandahimba Cooperative Bank Limited.**
9. **Azimio Maalum la kukasimisha mamlaka ya kusimamia na kutekeleza mchakato wa ufungwaji wa kampuni ya Tandahimba Community Plc kwa Bodi ya Wakurugenzi.**
10. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
11. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
12. **Kufunga Mkutano.**

**MAELEZO**

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 18/03/2024.*
2. *Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki ya Wananchi Tandahimba tarehe 15/03/2024 na kwenye Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU tarehe 19/03/2024.*
3. *Wanahisa watakaoshindwa kuhudhuria wana haki ya kujaza fomu ya uwakilishi iliyoambatanishwa.*
4. *Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.*

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**

**Katibu**

**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC,**
**Kiwanja Na. 49- Kitalu 'C', Barabara ya Namikupa,**
**S. L. P. 06, Tandahimba**
**Mtwara.**
**Namba ya Simu: +255 23 241 0093**
**Barua pepe: info@tacobabank.co.tz**

**KWA IDHINI YA BODI**

J. B. Rugambo
**KATIBU**

23 Machi, 2024



TEMBO NICKEL

## TAARIFA KWA UMMA

Kampuni ya Tembo Nickel inautahadharisha umma kuhusu uwepo kwa matapeli wa mtandaoni wanaotumia jina la Kampuni, jina la Mkurugenzi Mtendaji mkuu wa Kampuni, Bw. Benedict Busunzu, pamoja na majina mengine kwa lengo la kurubuni watu fedha kwa kuwaahidi fursa katika Mradi wa Kabanga Nickel.

Kampuni Vilevile imebainisha matapeli wa mtandaoni wanaotumia barua pepe feki za kutangaza fursa zinazofanana na barua pepe za kampuni ili kurubuni au kuchota taarifa za kieletroniki za walengwa.

Kampuni ya Tembo Nickel imeripoti matendo haya ya uhalifu kwenye mamlaka husika.

Ukiwa mlengwa na/au muathirika wa utapeli huu tafadhali toa taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu yako.

Kampuni ya Tembo Nickel haipokei fedha kwa lengo la kutoa fursa yoyote. Ni marufuku kwa mfanyakazi wa Tembo Nickel kupokea rushwa.

Kampuni ya Tembo Nickel, wafanyakazi na uongozi wote hautohusika na utapeli huu.

Tafadhali tambua kuwa, kampuni ya Tembo Nickel inapokea fursa kupitia barua pepe za tenders@kabanganickel.com pamoja na jobs@tembonickel.com isipokuwa tu pale njia mbadala itakapotangazwa rasmi. Kwa ajira za muda mfupi kwa wananchi wanaoishi eneo la Mradi, mchakato wa ajira hutolewa kupitia kanzi data maalum inayoshirikisha uongozi wa vijiji husika.

**IMETOLEWA NA MAMLAKA**




Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni (wapili kulia) akipokea sehemu ya tisheti 100 kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Same, Emily Mkende (watatu kushoto) ikiwa ni sehemu ya tisheti 100 zitakazo tumika kwenye maonyesho ya Same utalii Festival kama sehemu ya udhamini wa Benki hiyo pamoja na kutoa kiasi cha shilingi milioni tano. Makabidhiano haya yalifanyika katika ofisi ya mkuu wa Wilaya. **PICHA: MPIGAPICHHA WETU**

# Mataragio gumzo uteuzi, utenguzi vigogo

**Na Romana Mallya**

SUALA la uteuzi na utenguzi kwa wateule wa Rais Samia Suluhu Hassan ikiwa ni sehemu ya kuimarisha utendaji serikalini si suala geni tena. Hiyo ni kutokana na kuwapo kwa taarifa za namna hiyo ambazo zimekuwa zikitolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu.

Mara kwa mara, Rais amekuwa akitangaza uteuzi wa baadhi ya maofisa wa ngazi za juu wa serikali na taasisi zake, huku baadhi ya taarifa zikibainisha kuwa Rais ametengua uteuzi wa kigogo fulani. Inaishia hapo lakini wakati mwingine inaelezwa kuwa mtenguliwa huyo atapangiwa kazi nyingine.

Juzi usiku, Rais alimteua Dk. James Mataragio kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati kuchukua nafasi ya Athumani Mbuttuka, ambaye uteuzi wake umetenguliwa na kwamba atapangiwa kazi nyingine. Kabla ya hapo, Dk. Mataragio alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Uteuzi na utenguzi uliofanyika juzi ni mwendelezo wa Rais katika kufanya mabadiliko tangu alipoingia madarakani na ndani ya miezi sita, Rais amefanya mabadiliko ya namna hiyo huku Dk. Mataragio akiwa gumzo kila kona.

Agosti 18, mwaka jana, Rais Samia alitengua uteuzi wa Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba, ikiwa ni miezi sita tangu amteue kushika wadhifa huo. Siku 36 baadaye (Septemba 23, 2023) Rais alifanya uteuzi na kutengua viongozi mbalimbali, akiligusa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kugusa nafasi ya juu ya Mkurugenzi Mtendaji kwa kumteua Mhandisi Boniface Nyamo-Hanga.

Aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Maharage Chande, alipelekwa Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) akichukua na Mhandisi Peter Ulanga. Hata hivyo, alimrejesha Mhandisi Ulanga na Chande kumteua kuwa Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Januari 11, mwaka huu, alifanya uteuzi na kutengua baadhi ya viongozi akiwamo Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede.

Pia Februari 6, 2024, alifanya uteuzi uliogusa taasisi za kiuchumi; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

**KAULI ZA RAIS**

Rais Samia amekuwa akiweka wazi kila anapofanya mabadiliko ya uongozi akiorodhesha sababu zikiwamo kasi ya serikali, mabadiliko ya kawaida, kutoelewana bosi na wasaidizi huku akisisitiza kuwa hatua hiyo itakuwa endelevu.

Desemba 8, 2022 katika Mkutano Mkuu wa 10 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma, Rais Samia alisema katika safari yake aliyoianza Machi 19, 2021 anahisi ana watu ambao mwendo wao hauendani na kasi ya serikali yake.

"Ninawaomba sasa mnipe baraka zenu nikaipange serikali pia. Nikaipange serikali kwa jinsi ambavyo ninahisi timu hii (ya CCM) tunaweza kwenda kuyatekeleza yale mliyoyasema hapa kwa vizuri zaidi," alisema Rais Samia ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM.

Aidha, Februari 28, mwaka jana, alipowaapisha wateule wake, alitamka: "Nilidhani kuwa lile jeshi lililopo tungekwenda nalo mpaka tuvuke ule mwamba wa kuingia upande wa pili, katika safari ajali zinatokea mwingine anajikwaa anaanguka." Pia alitoa angalizo la kanuni ya uamuzi wake kwamba kuna wakati unakuwa wa kawaida katika kuimarisha utendaji serikalini, akatolea ufafanuzi anavyofanya mabadiliko mengi ya watendaji wakuu kisekta serikalini, yaani makatibu wakuu wa wizara. "Tumejitahidi kunyofoa katika maeneo mliyoko kujaza nafasi hizi, tukijua kuwa kila mtu anaelewa eneo lake alilopo.

"Tutaendelea kunyofoa huko na kuleta ndani ili atusaidie serikali kwa sababu akikaa nje kazi ni kulaumu tu, hajui ugumu uliomo ndani ya serikali, akiingia tutafanya nao watupe uzoefu wao waone yaliyopo serikalini ili twende kwa pamoja," alisema.

**SAFARI YA DK. MATARAGIO**

Dk. James Mataragio, ni miongoni mwa viongozi walioguswa na hatua hizo za Rais Samia kwa misamiati yote miwili "kuteuliwa" na "kutenguliwa" katika muhstakabali na mazingira tofauti. Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu, Rais Samia amemteua Dk. Mataragio kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, nafasi ambayo inampandisha ngazi.

Desemba 18, 2014, Dk. Mataragio aliteuliwa na Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC lakini. Agosti 20, 2016 alisimamishwa kazi na Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC na Julai 23, 2019, Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli, aliagiza arejeshwe katika nafasi yake.

Hata hivyo, Aprili 4, 2021, alitolewa TPDC na nafasi hiyo kuchukuliwa na Thobias Mwesiga aliyedumu si chini ya saa 12 na kutenguliwa, hivyo Dk. Mataragio kurejeshwa tena katika wadhifa huo kuanzia Aprili 5, 2021.

Safari ya Dk. Mataragio haikuishia hapo kwani Februari 24, 2023 alitenguliwa na kuteuliwa Mussa Mohamed Makame, huku taarifa ikisema (Dk. Mataragio) atapangiwa kazi nyingine.

Kabla ya kuwa mtendaji mkuu wa TPDC, Dk. Mataragio alikuwa anafanya kazi katika kampuni ya Marekani ya Bell Geospace, iliyoko Houston, Texas, akiwa Mwanajiolojia Mkuu kwa miaka 10. Mwaka 2014, alikuwa miongoni mwa Watanzania waliokubali kutii wito wa uzalendo na kuacha kazi yake na kurejea Tanzania ili kuleta utaalam wake na kufanya kazi katika taasisi ya umma.


## ABUMUSA FOREX BUREAU DE CHANGE

### POSITION-FOREX CASHIER (3)

We are looking for qualified and experienced cashiers to process cash transactions in national and foreign currencies. They provide information on the conditions and exchange rates for buying and selling foreign currencies, make deposits of money, record all foreign exchange transactions and check for money validity.

**Duties and Responsibilities**

- Ensure transactions are completed in an efficient manner with high level of accuracy.
- Maintain a cash float and follow balancing and reconciling procedures.
- Prepare daily 'End of Day' sheet at the close of each business day.
- Provide support and information to customers over the counter or by phone.
- Open/Closes office as required and ensure all tasks and checks are completed.
- Follow compliance procedures, company policies and abide by all health and safety guidelines as per requirements.
- Perform administrative tasks such as filling, generating reports and maintaining mail correspondence.

**Minimum Qualifications**

- At least 5 years' experience working in a forex exchange as a cashier.
- Diploma and above in accounting or other related fields.
- Integrity of the highest order.
- Competent in computer packages, i.e. excel, word etc.

Note: Applicants who meet the required qualifications to send their detailed CV's attached with a cover letter to **info@tenforce.co.tz or salimkabora94@gmail.com** on or before **27th February, 2024.**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**


# Mbivu, mbichi hukumu mke Bilionea Msuya leo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, leo inatarajiwa kutoa hukumu ya kesi ya mauaji inayomkabili mjane wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita, na mwenzake Revocatus Everist Muyella, maarufu kama Ray.

Mjane huyo kwa mara ya kwanza alipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, Oktoba 23, 2016 akidaiwa kumuua wifi yake, Aneth Msuya, aliyeuawa Mei 26, 2016 kwa kuchinjwa nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, mkoani Dar es Salaam.

Aneth alikuwa mdogo wa Bilionea Msuya, aliyeuawa kwa kupigwa risasi eneo la Mijohoroni, Hai mkoani Kilimanjaro Agosti 7, 2013. Katika utetezi wake, Mrita alidai kuwa hawezi kumuua Aneth kwa sababu alikuwa kama mtoto wake wa kuzaa kwa kuwa alipoolewa yeye na mume wake walikabidhiwa wamlee tangu akiwa shule ya msingi.

Hukumu hiyo inatarajiwa kutolewa na Jaji Edwin Kakolaki na hatua hiyo ilifikiwa baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa mashahidi 25 wa upande wa mashitaka, utetezi, vielelezo na kupitia vifungu vya sheria.

Desemba 11, mwaka jana wakati wazee wa baraza (Iddi Humba na Omary Panzi) wanatoa maoni yao, waliishauri mahakama iwaachie huru washtakiwa kwa madai kuwa hawana hatia.

Mzee Humba alidai kuwa amepitia ushahidi wa mashahidi 25 na ushahidi wa upande wa utetezi katika mashahidi watano wa utetezi, na kujiridhisha kwamba upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha shtaka bila kuacha shaka yoyote.

Jaji Kakolaki baada ya kusoma muhtasari wa ushahidi wa kila shahidi wa pande zote, alisema katika jinai kuna mambo makuu mawili ya kuangalia kitendo chenyewe ambacho mshtakiwa anakuwa anatuhumiwa kukitenda ni kwamba lazima kiwapo na kithibitike. Wakati shahidi wa 22 anatoa ushahidi wake, Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai Mkoa (RCO) wa Arusha, Mrakibu Mwandamizi (SSP) David Mhanaya, alidai kuwa Mrita alikuwa na ugomvi wa mali na wifi yake Aneth kwa sababu alianza kuuliza mali za marehemu mume wake.

Shahidi wa 25 wa upande wa mashitaka, Getruda Mfuru ambae alikuwa dada wa kazi wa Aneth alidai kuwa hakuwasaidia wahalifu kufanya uhalifu licha ya kwamba aliondoka nyumbani kwa bosi wake siku moja kabla ya tukio la mauji kutokea.

Hata hivyo, wakati Miriam anajitetea alidai kuwa hakuwahi kuwa na ugomvi wa mali na Aneth alikuwa akiishi nae vizuri hadi kufikia hatua ya kumuozesha, kwa hiyo alikuwa ni kama mtoto wake wa kumlea na pia anajua kama baba mkwe wake alikuwa na mgodi wa madini.

Pia mtoto wa marehemu Bilionea Msuya, Kevin, wakati akimtetea mama yake mzazi alidai kuwa baba yake alikuwa akimiliki gari moja tu na pia hana mali anazomiliki jijini Dar es Salaam na hiyo ilitokana na taarifa ya ukusanyanyi wa mali za marehemu baba yake kwa maelekezo ya mahakama.

Wakili wa Mrita, Peter Kibatala alidai mahakamani kuwa wanataarifa kuwa alikwenda mahakamani kutoa ushahidi kama dada wa kazi wa Aneth, Getruda Mfuru ni askari na kituo chake cha kazi ni Zanzibar.

# Mvua za masika zinatarajiwa kupunguza joto

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa utabiri wa mvua za masika ambazo zinatarajiwa kupunguza hali ya joto lililopo katika baadhi ya mikoa nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema jana kuwa mvua hizo zitarajiwa kuanza kunyesha kuanzia wiki ya mwisho ya mwezi huu na wiki ya kwanza ya Machi kwa baadhi ya mikoa.

"Mvua hizi tunatarajia zitakuwa za wastani mpaka juu ya wastani (mvua nyingi). Maeneo mengi yanayopata mvua misimu miwili kwa mwaka, tunashauri mamlaka na wananchi kuchukua tahadhari kwa athari zinazoweza kujitokeza.

"Kwa sasa tunafahamu maeneo mengi yanakabiliwa na hali ya joto, hivyo tunatarajia mvua hizi zitapunguza hali ya joto iliyopo sasa," alisema. Dk. Chang'a aliitaja mikoa itakayopata mvua hizo kuwa ni Dar es Salaam, Pwani, Kaskazini ya Morogoro, Tanga na visiwa vya Pemba na Unguja.

"Kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini inayojumuisha Arusha, Kilimanjaro na Manyara, tunatarajia mvua hizi zitaanza wiki ya mwisho ya Februari na kumalizika wiki ya pili na ya tatu ya Mei," alisema.

Mvua hizo pia zinatarajiwa kunyesha mikoa ya Kanda ya Ziwa ikijumuisha Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Kagera na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko) na zitaanza kunyesha wiki ya kwanza ya Machi na kukutana na mvua za nje ya msimu zinazoendelea kunyesha katika mikoa hiyo.

**ATHARI KUWAPO**

TMA imetahadharisha kutuama kwa maji katika maeneo mengi kutokana na mvua hizo na kushauri sekta mbalimbali kama afya kuchukua hatua kutokana na uwezekano wa kutokea magonjwa ya mlipuko.

"Tunatarajia pia mvua hizi zitaleta athari katika sekta ya usafiri na usafirishaji. Kunaweza kutokea uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli," alisema.

Dk. Chang'a alisema mvua hizo zitachangia kuongezeka kwa kina cha maji kwenye mabwawa na mito, hivyo sekta ya nishati inaweza kunufaika katika uzalishaji wa umeme.

Alishauri wananchi waendelee kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka hiyo kupitia vyombo vya habari ili kuchukua hatua sahihi.

# Manufaa ziara za Rais yaanikwa

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, wameeleza mafanikio yaliyopatikana kutokana na ziara zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika nchi mbalimbali.

Akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jana, Prof.Mkumbo alitaja manufaa hayo kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji ambao pia wameongeza ajira kwa makundi mbalimbali.

Prof. Mkumbo alisema kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2022 Tanzania ilivutia uwekezaji wa mitaji ya Dola za Kimarekani milioni 770 na kipindi kama hicho mwaka jana, iliongezeka hadi kufikia Dola milioni 1,396.

"Miradi iliyotiwa Saini katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2022 ilikuwa 58 lakini kipindi kama hicho mwaka jana, ilifikia miradi 213.

Kuhusu ajira, alisema Oktoba hadi Desemba, 2022 watu 10,216 waliajiriwa na na kipindi kama hicho mwaka jana, waliajiriwa watu 14,390.

"Uwekezaji ni mchakato. Rais Samia alifanya ziara China mwaka 2021 na kutokana na ziara hiyo, tayari tuna viwamda viliwi vikubwa sana. Mwaka jana, Rais Samia alizindua kiwanda kinachotengeneza vioo vya ujenzi Mkuranga na kiwanda cha nne kwa ukubwa katika bara la Afrika. sehemu kubwa ya kiwanda hicho wanauza nje.

"Kutokana na ziara hiyo, tulipata uwekezaji wa Sino-Tan Industrial Park ambayo iko Kwara, Kibaha ambayo uwekezaji wake ni zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 321 na uwekezaji wote utakapokamilika utakuwa Dola za Kimarekani bilioni tatu, sawa na Sh.trilioni 11, alisema.

Pia alisema ziara ya Misri imesaidia kuanzisha kiwanda cha kuzalisha transfoma, nyaya na vifaa vingine vya umeme kilichopo Kibaha mkoani Pwani huku akibainisha kuwa safari ya Indonesia, itafungua kiwanda cha mbolea mkoani Mtwara kitakachozalisha bidhaa hiyo kwa kutumia gesi asilia Pamoja na wawekezaji wa uzalishaji wa sukari,.

Katika ziara ya India, Prof. Kitila alisema wawekezaji kutoka nchi hiyo wanatarajia kuwekeza nchini katika viwanda vya kuunganisha matrakta kwa ajili ya wakulima.

"Kwa hiyo natoa mifano hii ili kwamba watu wajue matunda ya hizi ziara ambazo pia zinahamasisha hadi Watanzania kuweka," alisema Prof.Kitila.

Zuhura alisema alisema ziara hizo zimekuwa na manufaa makubwa kwa nchi akitolea mfano wa ziara ya Vatican ambako alikutana na Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis.

"Kwa ujumla ziara ilienda vizuri sana na kikubwa ilikuwa ya kuimarisha uhusiano wa Kidiplomasia na kimaendeleo ya nchi hizo mbili, na mnavyojua uhusiano upo kwa muda mrefu na unaenda vizuri,"alisema Zuhura.

Alisema katika mazungumzo na Kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki, walizungumzia pia amani na usalama duniani, mabadiliko ya tabianchi, demokrasia, utawala bora na haki za binadamu.

Mazungumzo mengine ya Rais Samia na Katibu Mkuu wa Vatican yalihusu masuala ya elimu, afya na huduma za maji ambayo tayari Kanisa Katoliki limeyapa kipaumbele na jinsi ya kuendelea kusaidiana katika maeneo hayo.

Zuhura alisema kuwa katika mazungumzo hayo, Rais Samia alipendekeza kuongezwe wigo wa maeneo mapya ya ushirikiano na Vatican ikiwamo uhamilishaji wa mafunzo ya ufundi stadi.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

## UNAUDITED RESULTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2023

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) continues to deliver strong operating results. Despite El Niño heavy rains in the last quarter of the year that impacted the distribution of cement and the overall results for the quarter, the Company managed to post good results for the year 2023 compared to year 2022. Revenue declined by 1% whereas the profit before tax grew by 2% year on year.

The overall performance is attributed to the product mix, process improvement and cost control in our production. Plant availability and efficiency also played a vital role to the improved performance in 2023.

The Company continues to focus on customer service and selling new products within our high quality portfolio. We maintain strong customer reationships which enabes TPCPLC to demonstrate its strength as the eading payer in the industry.

Prospects In spite of the cement demand slowing down this year, we are optimistic about the future. TPCPLC will continue to work on improving efficiency and operating performance.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

**BY ORDER OF THE BOARD**

**Hakan Gurdal**
**Chairman of the Board**

**STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2023**

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 490,171,829 | 494,716,182 |
| Cost of sales | (333,840,537) | (328,592,344) |
| Gross profit | 156,331,292 | 166,123,838 |
| | | |
| Other operating income | 9,745,144 | 841,677 |
| Selling and marketing expenses | (5,891,730) | (3,082,702) |
| Administrative expenses | (25,932,165) | (25,216,626) |
| Other operating expenses | (1,504,148) | (2,727,675) |
| Operating profit | 132,748,393 | 135,938,512 |
| | | |
| Finance income | 2,555,229 | 3,139,579 |
| Finance costs | (627,369) | (810,519) |
| Net gain on foreign currency translation | 8,795,331 | 1,829,994 |
| Profit before tax | 143,471,584 | 140,097,566 |
| | | |
| Income tax expense | (44,287,839) | (42,738,964) |
| Profit for the year | 99,183,745 | 97,358,602 |

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2023**

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| ASSETS | | |
| Non-current assets | | 142,330,100 |
| Property, plant and equipment | 138,410,187 | 813,318 |
| Intangible assets | 858,706 | 980,929 |
| Leasehold land | 953,086 | 4,333,991 |
| Right of Use assets | 1,004,266 | 574,000 |
| Other financial assets | 292,000 | |
| | 141,518,245 | 149,032,338 |
| Current assets | | 85,992,840 |
| Inventories | 91,456,317 | 53,561,114 |
| Trade receivables | 57,302,350 | 24,193,735 |
| Other short-term operating receivables | 18,450,522 | 600,000 |
| Other financial assets | 600,000 | - |
| Current income tax receivable | 2,454,136 | 105,512,644 |
| Cash and cash equivalent | 131,369,614 | |
| | 301,632,939 | 269,860,333 |
| | | |
| TOTAL ASSETS | 443,151,184 | 418,892,671 |
| | | |
| EQUITY AND LIABILITIES | | |
| Equity | | 3,598,462 |
| Authorised, issued and fully paid-up share capital | 3,598,462 | 296,139,811 |
| Retained earnings | 324,959,288 | |
| TOTAL EQUITY | 328,557,750 | 299,738,273 |
| | | |
| Non-current liabilities | | 1,149,572 |
| Lease liabilities | 185,766 | 5,339,322 |
| Employment benefit liabilities | 5,948,863 | 4,266,311 |
| Provision for quarry site restoration | 4,573,453 | 0,066585 |
| Deferred income tax liability | 10,559,788 | |
| | 21,267,870 | 20,821,790 |
| Current liabilities | | 3,461,375 |
| Lease liabilities | 963,806 | 521,690 |
| Current income tax payable | - | 78,394,395 |
| Trade and other payables | 78,853,764 | 13,049,775 |
| Provisions | 10,583,245 | 2,905,373 |
| Dividend payable | 2,924,749 | |
| | 93,325,564 | 98,332,608 |
| TOTAL EQUITY AND LIABILITIES | 443,151,184 | 418,892,671 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukosefu huduma ya maji Dar upatiwe ufumbuzi wa kudumu

**WANANCHI** katika mkoa wa Dar es Salaam, wamepaza sauti zao kuhusu hali ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo mbalimbali huku lawama nyingi zikitupwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Kwa mujibu wa wananchi hao, wamekumbana na uhaba wa huduma hiyo ambayo katika baadhi ya maeneo hawapati kwa zaidi ya mwezi sasa. Hata katika baadhi ya maeneo ambayo angalau wanapata kwa kusuasua, huduma hiyo inaweza kupatikana mara moja au mbili kwa wiki. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa maji ni mbaya katika maeneo mengi hususan mkoa wa Dar es Salaam.

Aidha, ukosefu wa huduma hiyo umesababisha baadhi ya wadadisi wa masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kuhoji kama hali hiyo inasadifu na ahadi ya serikali kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 kuwa upatikanaji wa maji utakuwa asilimia 95 kwa maeneo ya mijini.

Kukosekana kwa huduma hiyo kutoka katika miundombinu ya DAWASA, kumesababisha wananchi kutumia maji ya visima tena yasiyofaa. Hali hiyo pia imetoa fursa kwa wachuuzi kufanya biashara huku wananchi wakilalamika kununua kwa bei ya juu. Dumu la lita 20 linauzwa kati ya Sh. 600 na 700 huku katika baadhi ya maeneo kama Mbezi Msumi ikielezwa kuwa bei imepaa hadi Sh. 1,300.

Kilio cha namna hiyo kiko pia katika maeneo ya Tabata Kimanga, Segerea na Kinyerezi ambako imedaiwa kuwa ndoo ya lita 20 inauzwa kwa wastani wa 200 na 300 hudu dumu likiuzwa kwa Sh. 500. Pamoja na kuuzwa kwa bei hizo, maji hayo yana ukakasi kuhusu usalama wake kwa kuwa ni ya visima na mengine hayajulikani yanakotolewa kutokana na kuletewa nyumbani kwa mikokoteni na wachuuzi.

DAWASA pia iliwahi kujitetea kuwa kumekuwa na uhaba wa maji katika Mto Ruvu ambao ni tegemeo kubwa katika upatikanaji wa maji kutokana na shughuli za kibinadamu, zikiwamo kilimo na mifugo kuingizwa ndani ya rasilimali hiyo. Pia katika utetezi wake huo, DAWASA iliwahi kusema hali hiyo inatokona na uhaba wa mvua ambayo ilikuwa haijanyesha katika maeneo mbalimbali ambayo ni chanzo cha mto huo.

Jambo la kujiuliza ni je, mvua kubwa iliyonyesha hivi karibuni na kusababisha maafa katika baadhi ya maeneo haijawezesha Mto Ruvu kuwa na kiwango cha kutosha cha maji kuwezesha wananchi kupata huduma hiyo?


Kwa jumla, majibu ambayo yamekuwa yakitolewa na mamlaka hiyo si ya kuridhisha. Kwa lugha nyingine, ni majibu ya kisiasa zaidi kuliko uhalisia. Kwa hali hiyo, DAWASA inapaswa kujitafakari juu ya utendaji wake kwa sababu ilishaibuka na mipango mingi kama ujenzi wa bwawa la Kidunda na mradi wa visima virefu Kisarewe I na II.

Mbali na miradi hiyo, ilielezwa kuwa baada ya kusafishwa kwa visima hali ya maji itakuwa nzuri. Hali shwari hiyo ya upatikanaji wa maji itakuwa lini? Watu waendelee kuumia na kuwa katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu hadi lini?

Tatizo la maji katika mkoa wa Dar es Salaam si la sasa bali ni la muda mrefu, hivyo serikali kupitia Wizara ya Maji na DAWASA, haina budi kuchukua hatua za ziada katika kukabiliana na tatizo hilo ambalo limekuwa sawa na hadithi isiyo na mwisho.

Kama ni utendaji mbovu ndani ya mamlaka serikali ichukue hatua za kuwaondoa au kuwalioko katika nafasi hizo, wajiengue kuwapisha wengine wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kampeni chanjo Surua na Rubella, ina maana kubwa kwetu, tuiunge mkono

**MIAKA** ya hivi karibuni tumesikia sauti kutoka kila kona, serikalini, wadau na wasio wadau wakihimiza suala la chanjo.

Ni mada iliyopata kungwa mkono katika jamii zetu, hasa baada ya kuibuka maradhi ambayo hata nasi hatukuyatarajia, ukiwamo Uviko 19. Hata hivyo, utekelezaji wa chanjo katika jamii zetu kihistoria ina ukongwe.

Katika dhana 'maisha yaendelee', kinachotamba sasa ni wazazi na walezi wanatakiwa kujenga utaratibu wa kuwapeleka watoto wenye sifa za kupata chanjo, washirikishwe, ikiwa ni jambo linalosisitizwa.

Kimsingi, kunasaidia watoto kukingwa dhidi ya kupata magonjwa mtambuka. Inakuwaje kama mtoto asipopatiwa chanjo pale umri wake unapofika wa kupata chanjo? Ni wazi anaweza kuruhusu mwili huo kupata magonjwa kirahisi na baadhi ni ya hatari.

Hiyo ndio maana wataalamu wa afya katika kanuni zao za kazi hutaka chanjo hizo na hasa za msingi kufanyia mapema zaidi kumuepusha mtu kutapa maambukizi.

Pengine sina haja ya kufafanua sana chanjo hizo za msingi, kwa vile wengi tunazifahamu na tunapaswa kuzithamini.

Hata hivyo, kuna kila haja na sababu ya kuhakikisha watoto wanapatiwa chanjo ili kujilinda dhidi ya magonjwa hayo.

Kwa kutafakari katika kipindi cha mwezi huu, serikali imezindua kampeni ya chanjo ya kujihami na maradhi surua, pia rubella, tukiambiwa matarajio yaliyoko ni kwamba, jumla ya watoto zaidi ya 8,908,108, wanatarajiwa kupatiwa chanjo nchini.

Tunachopaswa kuelewa hasa sisi wazazi ni kwamba, magonjwa surua na rubella, yanazuilika kwa njia ya chanjo ya kwanza.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, imezindua Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo ya Surua - Rubella, ambao kwa nchi nzima wanatarajia kuwafikia watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kinga kutoka Wizara ya Afya, Dk. Tumaini Haonga, anatamka katika uzinduzi wa kampeni hiyo kitaifa, katika maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Haonga anasema, lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha wanazuia kuenea kwa ugonjwa surua na rubella, pia kuongeza kinga kwa walengwa,akiweka msisitizo usimamizi wa chanjo hiyo, kutokana na umuhimu wake, kwani inaongeza kinga kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Anasema, zaidi ya vituo 7,373 katika maeneo mbalimbali nchini vimetengwa kuhakikisha wanatoa huduma hiyo kikamilifu, ili kuweza kufikia lengo walilojiwekea.

Rai ya tabibu huyo ni kwamba, wakuu wa mikoa,wilaya na wanganga wakuu wa mikoa na wilaya, wahakikisha wanasimamia kikamilifu kuwapatia chanjo watoto wenye umri kuanzia miezi tisa mpaka 59 (chini ya miaka mitano)

"Niwaombe wazazi kutumia fursa hii kuwapeleka watoto wao waweze kupatiwa chanjo kwani ni muhimu kwa watoto kupata chanjo hiyo," anasema.

Ananivutia Daktari Haonga akisema, wamepata mrejesho tangu kuanza kwa chanjo zoezi hilo katika maeneo mbalimbali, wazazi wakijitokeza kwa wingi na wanaendelea kujitokeza kulinda afya za watoto wao.

Hapo wazazi katika nafasi zetu, tunapaswa kuelewa ni nafasi yetu kukabili utata huo ambao ukiachiwa kumea, unaathiri sana afya ya watu katika namna mbalimbali.

Vilevile, katika namna tunavyotekeleza katika jamii zetu, inafungua picha fulani yenye utamaduni ndani yake, kwamba wajifunze kuwajibikia chanjo iwe mpya au iliyozoeleka, yaani zile kongwe.

Wakati huohuo, pia inafungua sura ya kuwaunga mkono wasimamizi kutoka serikalini, juu ya namna gani inafanywa katika mtiririko wa ufanisi.

Hata katika tafsiri hiyo hiyo, sababu ya kuwapo Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), inayoumba muundo wa jamii kuwa na zahanati, vituo vfya afya hadi hospitali za ngazi mbalimbali na huduma zake katika maeneo hayo, ni hii kampeni inahusika.

Maana mojawapo ni majukumu kama hayo ya chanjo na tiba kwa ujumla, imebeba maana hizo. Sasa tukitangaziwa chanjo na yanayofanana nayo, kisha hatutumii, tunakuwa kama vile tunaisaliti MMAM tuliyoishangilia ilipoanzishwa.

## HABARI KITAIFA

# Vijiji 108 vyapata umeme toka REA

**Na Mwandishi Wetu**

VIJIJI vyote 108 vya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe vimeshafikishiwa umeme kupitia miradi inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa gharama ya Sh. bilioni 9.5 .

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayi juzi akiwa katika ziara ya kikazi wilayani humo. Aliyasema hayo katika Kijiji cha Ikwavila katika hafla ya kuwasha umeme katika Shule ya Msingi Ikwavila

Mbunge wa Wanging'ombe ambaye pia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alikiri na kuipongeza serikali kupitia Wizara ya Nishati na REA kwa kuvifikishia umeme vijiji nishati hiyo.

"Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kati ya vitongoji 525 tulivyo navyo, watendaji wako wachapakazi tayari wametuletea umeme katika vitongoji 295," amesema.

Dk. Dugange alisema katika Mwaka huu wa fedha, serikali imeanza utekelezaji wa miradi ya REA katika vitongoji vingine 72 huku 158 vilivyobaki vikiwa na makandarasi ambao wanaendelea na kazi.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema kwa sasa REA inatekeleza miradi mitatu katika maeneo tofauti Wanging'ombe.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili, Mradi wa Ujazilizi Fungu la Pili B na mradi wa kupeleka umeme kwenye vituo vya afya na pampu za maji.

Kuhusu takwimu za mkoa wa Njombe, alisema vijiji 361 kati ya 381 vimekwishafikishiwa umeme wa REA, sawa na asilimia 94.75.

Pia alisema vitongoji 1,148 kati ya 1,836 sawa na asilimia 62.5 tayari vimefikiwa na umeme kupitia miradi mbalimbali ya REA.

# Askofu matatani madai kupinga chanjo

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MKUU wa Wilaya ya Sumbawanga, Nyakia Chilukile, ameagiza kukamatwa kwa Askofu wa Kanisa la Zion Whatchtower, Abel Machofya, na kufungwa kwa kanisa hilo kwa madai kuwa limekuwa likiwakataza waumini wake kuwapeleka watoto wao kupata chanjo.

Agizo la kufunga kanisa hilo alilitoa juzi baada ya kwenda katika kijiji cha Lula, kata ya Kanda yaliko makao makuu ya kanisa hilo kwa nia ya kuwakamata viongozi wa kanisa hilo kutokana na kupinga baadhi ya maagizo na mipango ya serikali katika sekta ya afya.

Chilukile alisema kanisa hilo lenye wachungaji saba, akiwamo askofu huyo, limekuwa likitoa mafundisho potofu ikiwamo kuwakataza waumini kuwapeleka watoto kupata chanjo mbalimbali na hivi karibuni pia waliwazuia kupata chanjo ya Surua Lubela ambayo inaendelea kutolewa maeneo mbalimbali nchini.

Mkuu huyo wa wilaya alisema katika kipindi cha Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka juzi, kanisa hilo pia liliwazuia waumini wao kuhesabiwa hali ambayo ilisababisha mgogoro baina ya waumini hao na serikali.

Chilukile alisema pia waumini wa kanisa hilo ni marufuku kutumia simu za mkononi huku wakiambiwa ni dhambi na kwa yeyote atakayekaidi mafundisho hayo hataingia mbinguni.

"Naagiza kuanzia sasa kanisa hili la Whatchtower ni kuwepo kijijini hapa. Naagiza lifungwe mara moja na polisi kata mkamate huyu askofu wao. Pia muwasake na wachungaji wapakieni kwenye gari wapelekeni polisi sasa hivi," aliagiza Chilukile.

" Hawa nasikia mwaka jana wamegoma kuhesabiwa, wakakataa kuchanjwa chanjo ya polio na saa hizo wanakataa chanjo ya Sulua Lubera. Hatuwezi kuruhusu watu kuishi maisha ya kijima, naagiza hili kanisa lifungwe kabisa sitaki kuliona tena,"alisema.

Awali, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Yahya Msuya, alimwambia mkuu huyo wa wilaya kuwa wafuasi wa kanisa hilo wamekuwa wakigomea chanjo mbalimbali, hivyo kurudisha nyuma jitihada za serikali katika kukabiliana na magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa njia ya chanjo. Alisema katika kata ya Kanda, kijiji Cha Lula, kuna vitongoji vitano ambavyo vina waumini na kaya zipatazo 100 ndizo zinaabudu katika kanisa hilo na ndio wamekuwa na msimamo mikali dhidi ya baadhi ya huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Thomas Apson akizungumza jana na wananchi wa kijiji cha Misughaa kata ya Misughaa kutoa elimu ya namna ya kuchukua tahadhari kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu ambao umelipuka katika wilaya hiyo. **PICHA :THOBIAS MWANAKATWE**

# Mwendokasi sasa yanukia Kibaha- Moro

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amesema mipango ya serikali ni kujenga barabara ya mwendokasi (Express way) kuanzia Kibaha - Chalinze - Morogoro mpaka makao makuu Dodoma.

Bashungwa alisema hayo wakati akizugumza na waandishi wa habari alipokutana na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, kabla ya kuanza ziara yake ya siku nne mkoani hapa.

Alisema kujengwa kwa barabara ya mwendokasi kutoka Kibaha ambako barabara hiyo imeishia kutoka Kimara, Dar es Salaam hadi Kibaha iko katika mipango ya serikali.

Waziri Bashungwa alisema katika maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hasaan kwenye Barabara, ni kuona Dar es Salaam kama mji wa kibiashara inaunganishwa kupitia Morogoro na makao makuu ya nchi, Dodoma.

"Utaona upande mmoja kuna SGR (reli ya kisasa) na upande mwingine kuna barabara ya mwendokasi inayounganisha Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Kwa wana Morogoro hii ni neema kubwa kwa sababu shughuli za kilimo zitazidi kushamiri," alisema.

Waziri Bashungwa alisema mkoa wa Morogoro una wakulima hodari na kwenye kikapu cha mchango wa taifa kwenye uzalishaji wa chakula, mchango wake ni mkubwa.

"Yote hayo ni ni maelekezo ya Rais kwa vile mkoa wa Morogoro ni wa kimkakati kwenye kilimo. Maelekezo yake ni kuendelea kuiunganisha Morogoro na dunia kwa kuboresha miundmbinu ya barabara," alisema.

Bashungwa alisema kila mkulima wa mkoa wa Morogoro atajivunia kwamba akilima mazao yake anajua kuna miundombinu bora ya usafirishaji kwa kutumia reli ya mwendokasi au barabara .

"Morogoro ya kesho ni Morogoro itakayokuwa imekaa kimkakati na Rais Samia anazidi kuboresha miundombinu ili mkoa huu uzidi kuwa wa kimkakati katika kuendelea kusaidia uchumi wa nchi kupitia kilimo," alisema.

Bashungwa pia alisema kutokana na maono ya Rais ya utalii baada ya kutembelea wilaya za mkoa huo, atakutana na kukaa na waziri mwezake wa maliasili na utalii, Angellah Kairuki, ili kuangalia kwenye mbuga za wanyama ya Mikumi, Udzungwa na ya Mwalimu Nyerere namna ya kuboresha barabara za kwenda huko.

"Tunataka kuona kinachopangwa Wizara ya Utalii na Maliasili na sisi upande wa Wizara ya Ujenzi tunafanana. Kwa hiyo Mkuu wa mkoa hapa unatuambia Morogoro sio kilimo peke yake lakini hata kwenye utalii ni potential kubwa sana " alisema Bashungwa.

Malima alimwomba Waziri Bashungwa pamoja na mipango na mikakati ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, kuupa mkoa kipaumbele cha ujenzi wa makalavati ili kuziwezesha barabara hasa wiayani kupitika kipindi chote ili huduma za kijamii na kiuchumi ziendelee.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**



# Morogoro kuvuna maji ya mvua kukabili mafuriko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima amesema mkoa huo umewasilisha mapendekezo Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu kusaidia kudhibiti maji ya mvua yanayosababisha mafuriko.

Udhibiti huo umelenga kuyavuna maji kwa kuhifadhi kwenye mabwawa ili yatumike kwenye shughuli za kijamii na kiuchumi.

Malima aliyasema hayo wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama cha Mapinduzi (CCM), Februari 5, 1977 yaliyofanyika kimkoa mjini Morogoro, mgeni rasmi akiwa Mlezi wa CCM mkoani na Mwenyekiti wa Taifa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM), Mohamed Ally Kawaida.

Alisema kutokana na mafuriko yaliyojitokeza hivi karibuni na kuleta madhara, serikali ya mkoa imepeleka mapendekezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhangama alipofika mkoani Morogoro kujionea hali halisi ya athari za mafuriko yaliyosababisha madhara kwa wananchi. "Mvua iliyosababisha mafuriko katika miaka miwili ya hivi karibuni imekuwa ikiongezeka kwa kasi sana kwenye wilaya zote za Mkoa wa Morogoro, zimeathirika na mafuriko na imetokea kwa siku moja wilaya karibu nne zilikubwa na mafuriko," alisema Malima. Mkuu wa Mkoa alisema mafuriko hayo yameleta athari ya mali, mashamba yenye mazao na kupoteza uhai wa binadamu kwa kiasi kikubwa.

Malima alisema kwa ujumla katika mafuriko yote hayo kwa miezi mitatu iliyopita, mkoa umepoteza karibu watu 20.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imepanga kugharamia mafunzo ya muda mfupi ya ujuzi wa uokoaji kwa vijana zaidi ya 74 wa Fire Volunteer ambayo yatapangwa siku za usoni kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro.

Malima alisema hayo alipokabidhi fedha Sh. milioni 1.6 kwa vijana hao ikiwa ni kutimiza ahadi yake kutokana na kazi kubwa walioifanya ya kujitolea kwenye uokoaji watu na mali nyakati za mafuriko ya Januari 25, mwaka huu yaliyotokea maeneo mbalimbali ya mkoa ikiwamo Manispaa ya Morogoro.

"Kwenye mafuriko ya siku ile pale nikakuta kuna watu Volunteers wa zimamoto na uokoaji wa kujitolea lile jambo binafsi likanipa faraja kubwa nilisema nitatoa Sh. milioni moja mkapate hata sabuni kwa wale vijana 33 waliokuwapo pale," alisema.

Malima alisema vijana hao wanaojitolea katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji waliounga mkono uokoaji watu na mali zao baada ya kutokea mafuriko ya Januari 25, 2024 katika Manispaa ya Morogoro.

Mkuu wa Mkoa pia aliwaasa vijana hao kuwa na nidhamu, maadili mema, utayari na kutambua kuwa jambo hilo ni la kujitolea husasan katika kipindi chote watakachokuwa kwenye mafunzo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Shabani Marugujo alisema lengo la kuanzisha askari wa kujitolea wa Zimamoto na Uokoaji (Fire Volunteers) ni kutokana uwezekano wa kutokea kwa majanga ya moto na mafuriko.

Marugujo alisema majanga hayo yanasababishwa na kukua kwa teknolojia, ongezeko la watu na ukuaji wa miji na mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni muhimu vijana hao kuwa nao ili kuongeza nguvu katika uokoaji.



Wavuvi wa samaki wa mjini Bagamoyo mkoani Pwani, wakizifanyia matengenezo nyavu zao kwa kuzishona juzi, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kwenda baharini kuvua. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Uamuzi rufani kigogo wa TUICO Aprili

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Aprili 15, 2024 inatarajia kutoa hukumu ya rufani iliyokatwa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara na Taasisi za Fedha na Huduma (TUICO), Boniface Nkakatisi, kupinga uamuzi wa Mahakama ya Wilaya Ilala kutupilia mbali ombi lake la kutaka alipwe Sh. milioni 200 kwa madai ya kudhalilishwa na mwanachama.

Nkakatisi alikimbilia mahakamani kumshtaki aliyekuwa Mwenyekiti wa TUICO wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) tawi la Mikocheni, Mambo Mkufu, kwa madai kuwa aliandika barua ya kumkashifu na aliandaa mkutano wa waandishi wa habari kisha kumdhalilisha.

Kutokana na madai hayo, Nkakatisi aliiomba mahakama imwamuru Mkufu kumlipa fidia ya Sh. milioni 200 lakini Agosti 3, 2023 mahakama hiyo ilitupilia mbali madai hayo. Katibu mkuu huyo hakukubaliana na uamuzi huo ndipo alikata rufani Mahakama Kuu.

Rufani hiyo iliitwa jana mbele ya Naibu Msajili, Sundi Fimbo, kwa ajili ya kutajwa na kuangalia kama pande zote mbili zilikamilisha maagizo ya mahakama ya kuwasilisha hoja zao kwa njia ya maandishi.

Hatua hiyo ilifikiwa na mahakama baada ya Wakili wa Nkakatisi, Matthew Kabunga, kuiomba mahakama hoja ziwasilishwe kwa njia ya maandishi. Fimbo alimwuliza Mkufu kuhusiana na suala hilo akadai kwamba hana pingamizi.

Kutokana na kutokuwapo na pingamizi, Fimbo aliwataka hoja zao waziwasilishe Desemba 28,2023 na mjibu rufani (Mkufu) awasilishe majibu ya hoja hizo kwa njia ya maandishi Januari 11,2024 na kama kutakuwa na nyongeza ya hoja yoyote mkata rufani atawasilisha Januari 18, 2024.

Akitoa uamuzi huo katika kesi hiyo ya madai ya kashfa namba 79 ya mwaka 2021, Hakimu Mkazi Mwandamizi Rehema Lyana alisema mlalamikaji hakuwasilisha ushahidi wowote wa kuthibitisha madai hayo.

Pia alisema hakuna ushahidi unaoonyesha au kuthibitisha mlalamikaji alivyoteseka ili kuiwezesha mahakama hiyo kumpatia hasara ya jumla kama ilivyoombwa.

Hakimu Lyana pia alisema kupitia barua hiyo hakuna mahali inayoonesha kuwa Mkufu alimkashifu mlalamikaji kwenye vyombo vya habari, kwenye maofisi, vyombo vya usalama na magazeti.

Katika hati ya madai, Nkakatisi anadai kuwa Mkufu ambaye ni mwanachama wa TUICO kutokana na ajira yake TANESCO, Julai 19, 2021 kwa nia ovu na bila kuwa na sababu halali, alisababisha kuchapishwa kwa maneno yenye kashfa dhidi yake.

## Madiwani wagomea ripoti ujenzi VETA

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MADIWANI wa Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani, wamekataa kupokea taarifa ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kinachojengwa katika kijiji cha Magome kata ya Pera.

Wamekataa taarifa hiyo kwa madai kwamba mradi huo unasuasua huku fedha nyingi zikiwa zimetumika tofauti na ilivyo katika maeneo mengine ambayo yamenufaika na mradi kama huo.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika jana mjini hapa, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo, alitoa maelekezo kwa vyombo vinavyoshughulika na rushwa kufuatilia maendeleo ya mradi huo.

"Tunaagiza taarifa ikaandaliwe upya na iletwe kwenye kikao. Kuna taarifa ya Sh. milioni 300 zinetumika katika ujenzi wa chuo hiki lakini hata jamvi halijafunikwa mpaka sasa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, akizungumzia suala hilo alisema ushirikishwaji wa ujenzi wa chuo hicho umekuwa hafifu huku akieleza kwamba fedha nyingi zinetumika lakini mradi hauonekani.

"Mradi huu uko kwenye halmashauri yetu na umekuwa ukisuasua. Fedha zinapokuja inatakiwa zifanye kazi kwa haraka. Suala hili nimelipokea na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya anayehusika pia inatakiwa aandae mazingira Madiwani wakakague mradi huu," alisema Okash.

Mdhibiti Ubora na msimamizi wa mradi huo, Davis Moye, akizungumzia kukataliwa kwa taarifa yake, alisema shughuli za awali za ujenzi zilianza Julai, mwaka jana, zikisimamiwa na mhandisi elekezi kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salam (DIT).

Moye alisema baadaye kazi hiyo ilishindwa kuendelea kwa muda kutokana na kukosekana kwa majibu ya vipimo vya udongo, kazi iliyofanywa na Chuo Kikuu cha Ardhi na kushindwa kukabidhi ripoti kwa mshauri elekezi jambo lililochelewesha kuanza kwa ujenzi.

Kwa mujibu wa msimamizi huyo, Juni 29, mwaka jana, walipokea Sh. 228,942.380 awamu ya kwanza na Septemba walipokea Sh. 7,562.759 kwa ajili ya usimamizi. Pia alisema Desemba, mwaka jana walipokea Sh. 95,751,863.01 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji kwa ajili ya hatua zingine za ujenzi.

Mradi huo ambao ulikadiriwa kukamilika Februari, mwaka huu, kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 35.44 na hadi kukamilika unatarajiwa kutumika Sh. bilioni 1.5.





# Tani 400 za alizeti kuvunwa, kuingizwa sokoni

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAKULIMA 3,200 wa alizeti mkoani Manyara wanatarajia kuingiza sokoni mwishoni mwa msimu ujao tani zaidi ya 400 ili kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya kula nchini.

Mahitaji ya mafuta ya kupikia nchini kwa mwaka ni wastani wa tani 600,000 hadi 700,000.

Uzalishaji mdogo wa mafuta ya kupikia nchini umekuwa ukichangia bei kuwa kubwa ya mafuta yanayozalisha nchini kuliko yale yanayoingizwa kutoka nje ya nchi.

Akizungumzia mpango huo jana, Katibu Mtendaji wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti, Mkoa wa Manyara (MASUPA), Julian Kambayta, alisema tani 100 za awali zitavunwa na wakulima ambao mazao yao yameathiriwa na maji mengi.

"Tani 400 ndizo tunatarajia kuvuna msimu ujao, ambao ndio tumeanza kupanda. Tani 100 zitavunwa kwa wakulima wa awali, ambao wamekumbwa na maji mengi na tani 300 ni wale wanaopanda sasa hivi,"alisema Kambayta.

Aidha alisema kitu kinachowasaidia wakulima wa alizeti kuzalisha kwa tija ni uwezeshaji wanaopata kutoka Shirika la Farm Africa na baadhi ya kampuni za mbegu, kuwawekea mashamba darasa.

Kambayta alisema serikali imewawekea ruzuku kwenye mbegu ya 'record' ambayo inawapa punguzo la bei kutoka Sh. 30,000 mpaka Sh. 10,000 au Sh. 7,000 kwa mfuko mmoja katika baadhi ya maduka.

Aidha, akizungumzia mpango huo, Meneja Miradi wa Shirika la Farm Africa-Tanzania, Tumain Elibariki, alisema wanawezesha wakulima kwenye mradi wa farm to market alliance, ambao ndani yake kuna zao la alizeti.

Meneja huyo alisema kwa sasa wanawasaidia kuwepo na mashamba darasa, vituo vya huduma kwa wakulima ambavyo vinaratibu wakulima kupata pembejeo. Alisema wanawasaidia wakulima kupata masoko na wapo katika wilaya za Babati, Hanang', Kiteto na Simanjiro.

Ofisa Kilimo wa mkoa huo, Samweli Dahaye, alisema msimu wa 2022/23 mkoa ulizalisha tani 151,086 za alizeti na kusaidia bei ya mafuta kushuka kutoka lita moja Sh. 7,000 mpaka Sh. 4,000.

Dahaye alisema msimu ujao wa mwaka 2023/24 mkoa unatarajia kuzalisha tani 270,767 za zao hilo.



Mbunge wa zamani wa Arusha mjini na Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini, Godless Lema, akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha jana kutangaza maeneo rasmi watakayopita katika maandamano yatakayofanyika Februari 27 mwaka huu. **PICHA:GETRUDE MPEZYA**

# 80% ya watumishi sekta ya afya ni wanawake, hawajiamini

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia afya, Dk. Wilson Mahera, amesema asilimia 80 ya watumishi wa sekta hiyo ni wanawake.

Amesema wengi wao siyo wajasiri na kuna wakati wanashindwa kujiamini wanapopewa madaraka.

Kutokana na hali hiyo amewasihi wawanawake wanaopewa madaraka hasa nafasi za uongozi kujiamini kwa kuwa asilimia kubwa wanapopewa uongozi hufanya vizuri.

Dk. Mahera alieleza hayo jana jijini Arusha, alipokuwa akifungua semina ya siku mbili ya watafiti wa mradi wa kuleta usawa wa kiongozi katika mfumo na miundombinu kwenye sekta ya afya.

Kwa mujibu wa Dk. Mahera mradi huo unahamashisha wanawake kushika nafasi mbalimbali katika sekta ya afya.

"TAMISEMI inaunga mkono jitihada hizo na inawataka wanawake kujitoa na kuwa wajasiri na kujiamini katika shughuli za kiutendaji ili wawe viongozi bora baadae.

...Wanawake wana uwezo wa kuongoza wakiwezeshwa, na TAMISEMI imeona ni jambo jema kuwajengea uwezo wanawake kushika nafasi mbalimbali katika sekta ya afya, kwa vule wanajituma na hawasukumwi katika utendaji kazi wa kila siku."

Dk. Mahera, alisema katika halmashauri zote nchini waganga wafawidhi katika vituo vya afya, wengi wao ni wanawake, lakini hawajiamini licha ya kushika nafasi hizo kwa muda mrefu.

Mwanzilishi wa mradi huo, Prof. Henry Mollel wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, alisema mkakati wa kitaifa ni kupata uwakilishi mzuri wa kinamama katika sekta ya afya, kwani watendaji wakubwa katika sekta hiyo ni wanawake.

Prof. Mollel alisema mradi huo unalenga katika kutekeleza malengo ya serikali ya kutaka wanawake waliojiendeleza kushika wadhifa mbalimbali serikalini hususani sekta ya afya ambayo asilimia kubwa inaendeshwa na wanawake.

Alisema semina hiyo kwa kuanzia imeanza kwa kuwapa ujasiri wa kiongozi wanawake wa sekta ya afya kutoka mikoa mitatu ambayo ni Kilimanjaro, Kagera na Njombe, lengo ni kufanya semina katika sekta hiyo kwa mikoa yote nchini.

Msimamizi mkuu wa mradi, Dk. Anosisye Kasela, alisema lengo kuu la mradi ni kutatua malengo yanayokwamisha wanawake kupata uongozi sekta ya afya na serikali, hivyo semina hiyo inawapa uzoefu ili waweze kujiamini na kuwa wajasiri pindi wanapopata uongozi.

# Wajumbe shule KKKT watakiwa kufanya ukaguzi wa kushtukiza

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIBU wa Elimu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Peter Kithyaka, amewataka wajumbe wa bodi za shule za kanisa hilo kufanya ukaguzi wa kushtukiza shule zake za sekondari ambazo hazifanyi vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Amesema kufanya hivyo kutasaidia kanisa kubaini matatizo yanayotishia ubora wa shule zake na kuzitatua kwa haraka ili zing'are katika mitihani ya kitaifa.

Kithyaka alitoa maagizo hayo jana katika kikao kazi kilichowajumuisha pia wakuu wa shule zinazomilikiwa na KKKT, Dayosisi ya Kaskazini.

Mbali na kuweka mkakati wa kuongeza ufaulu, pia walijadili mambo mengine ikiwemo suala la kufanya kazi kwa bidii na kufuata misingi ya utawala bora.

Alisema: "Nawakumbusha kuwa wajumbe wa bodi, kwamba mnayo mamlaka ya kukagua shule kujiridhisha...kwamba shule uliyokabidhiwa kuisimami inakwendaje? Tukiwa makini na kujituma, shule zetu zitafanya vizuri na tutatoa huduma ya elimu iliyo bora kwa watoto wetu na jamii kwa ujumla."

Alisema pia wanapaswa kufanya tathimini ili waweze kujua jambo linalohitajika kufanyika kwa shule na taasisi wanazoziongoza za Dayosisi ya Kaskazini, ili ziweze kufanya vizuri katika kutoa huduma zenye ushindani.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge (MWECAU), Dk. Catherine James, ambaye ni mbobezi wa masuala ya uongozi na utawala, alisema uongozi ni kuwezesha watu na kuwasaidia watu kufanya yale wanayopaswa kufanya.

Dk. Catherine alisema malengo hayo ni yale yaliyowekwa na taasisi; na ni vyema kufahamu uongozi ni kuwaelekeza na kuwashawishi watu kufanya kazi na kufikia malengo ya taasisi.

Alisema kiongozi anapaswa kuwa na ushawishi, kuonyesha njia, kufanya maamuzi na ni mtu anayeweza kujituma.

Mhadhiri Mwandamizi wa MWECAU, Dk. Emmanuel Kileo, alisema katika aina hizo za uongozi inapendeza zaidi kuchagua aina ya uongozi katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia mazingira.

Dk. Kileo alisema sifa za kiongozi bora ni uadilifu asiyeyumbishwa, awe mfano bora na uwezo wa kushawishi na kuhamasisha watu anaowaongoza kufikia malengo.





# Kamati ya Bunge yatoa maagizo saba mgodi wa madini North Mara

**Na Timothy Itembe,** MARA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imetoa maagizo saba kwa mgodi wa North Mara Nyamongo na kuutaka kuyatekeleza kwa wananchi, ili kuhakikisha wanawekа uhusiano sawa na kudhibiti migogoro na kero zilizopo.

Maagizo hayo yalitolewa juzi na Mwenyekiti wa kamati hiyo, David Mathayo, wakati wa ziara ya kutembelea na kukagua shughuli zinazotekelezwa na mgodi huo sambamba na uwajibikaji wake katika jamii.

Alisema wakati wa ziara hiyo walibaini upungufu katika mambo mbalimbali ikiwemo uchafuzi wa mazingira na kuwataka kuimarisha uhusiano kwa jamii inayowazunguka ili kuhakikisha wanatekeleza ipasavya majukumu yao.

"Niwatake ndugu zangu kuzingatia utunzaji mazingira, kutoa gawio la Serikali pamoja na huduma kwa jamii kwa kuzingatia kanuni iliyotungwa ya mgawanyo wa fedha sawa na asilimia 40 kwa vijiji vinavyozunguka mgodi na asilimia 60 kwenye kata nyingine," alisema Mathayo.

Alisema maeneo ambayo yamefanyiwa thamini lakini hawana tena haja nayo wayatenge na kuwapa wananchi wazawa wakachimbe, vilevile waliofanyiwa tathimini wapewe karatasi ya udhamini ili kuondoa sintofahamu na kulipa fedha za wale ambao bado hawajalipwa.

Pia aliutaka uongozi wa mgodi huo kutoa ajira kwa kuzingatia agenda ya kutoa fursa kwa wazawa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii, ili waelewe manufaaa ya uwepo wa mgodi huo.

Makamu Mwenyekiti kamati hiyo, Kilumbe Ng'enda alikemea vitendo vya baadhi ya vijana wasiokuwa waaminifu ambao wanavamia mgodi kwa lengo la kuiba mawe yanayodhaniwa kuwa na dhahabu.

Meneja wa mgodi huo, Apolinary Lyambiko alisema watazingatia maelekezo yote yaliyotolewa na kamati, ili kuboresha utekelezaji wa shughuli za uzalishaji na kujenga uhusiano mzuri na jamii inayowazunguka.

Mkuu wa Mkoa Mara, Said Mtanda aliomba Wizara ya Madini kuona umuhimu wa kupanga ziara rasmi siku nyingine ya kutembelea wachimbaji wazawa wa madini kwa lengo la kuwapa elimu.



Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa akitoa maelekezo kwa viongozi wa chama hicho wa Wilaya ya Kahama kuhusu usimamizi wa zahanati ya kijiji cha Bukoba kata ya Isagehe na ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya, Mboni Mhita jana. **PICHA: SHABAN NJIA.**

## Mapato kiduchu 'yamliza' Mkurugenzi wa Halmashauri

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Kisena Mabuba, amesema kwamba hali ya ukusanyaji mapato katika halmashauri hiyo ni mbaya.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo na kutaja hali ya ukusanyaji mapato kutokuridhisha na kuwataka kuongeza usimamizi makini wa vyanzo vya mapato.

Hivyo aliwataka watumishi hao wakiwamo watendaji kata na maofisa kilimo, kuhakikisha wanadhibiti upotevu wa fedha katika maeneo yao ya kazi.

"Hali ni mbaya, mtu yeyote anayekiuka utaratibu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali mkamateni, haiwezekani halmashauri yetu kutofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato." alisema Mabuba.

Vilevile aliagiza kufanyika kwa ukaguzi wa mashine za ukusanyaji mapato ambazo hazifanyi kazi, pamoja na kununua mashine mpya ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Katika hatua nyingine alimwagiza Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Edward Maduhu, ahakikishe anasimamia vizuri vyanzo vya mapato katika idara hiyo kutokana na kuwa idara yenye vyanzo vikubwa vya mapato na inategemewa katika halmashauri hiyo.

Alitaja pia mikakati ya kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato ya halmashauri hiyo, kwamba ni kufuatilia na kufanya ukuguzi wa mara kwa mara wa kushtukiza ili kuziba mianya ya wizi, kuandaa kanzi data ya wafanyabiashara wote, kuongeza mashine za ukusanyaji mapato na kutoa elimu kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kulipa mapato.

Baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo, waliahidi kutekeleza maagizo hayo ikiwa ni jitihada za kurudisha hali nzuri ya mapato, fedha ambazo zitakwenda kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## RC Mara atoa siku 20 maji kupatikana kwa wananchi

**Na Vitus Audax,** BUTIAMA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda ametoa siku 20 kwa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mgango-Kiabakari kuhakikisha wanakamilisha mradi wa kupeleka maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea na kukagua ofisi ya mamlaka hiyo iliyopo eneo la Sabasaba wilayani Butiama na kueleza kuwa wananchi wamechoka taarifa na maelezo ya mara kwa mara na kwa sasa wanahitaji maji ya uhakika.

"Mimi na wananchi wa Butiama tumechoka taarifa nzuri za maendeleo ya mradi kwa sasa kinachohitajika ni maji safi na salama kutoka katika mradi huu uliotumia fedha nyingi kutekelezwa kwa zaidi ya miaka mitatu," alisema Mtanda.

Aidha aliahidi kufanya mazungumzo na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ili wapeleke vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya mradi huo kuanza kufanyakazi mapema na kusukuma maji ili kuwasaidia wananchi kuondokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo Mhandisi Cosmas Sanda alisema unatekelezwa kwa gharama ya Sh.bilioni 70.5 na kwa kwa sasa umefikia asilimia 97 ya utekelezaji wake.

Mhandisi Sanda alisema majaribio ya mitambo ya kusukuma maji kutoka kwenye chanzo hadi kwenye matangi unasubiria TANESCO wakamilishe kufunga umeme walioahidi kumaliza shughuli hiyo ndani ya siku 14.

"Mpango kazi na mkakati uliopo kwa sasa ni wananchi wa wilaya za Musoma, Bunda na Butiama kuanza kupata maji baada ya TANESCO kukamilisha ufungaji wa umeme katika maeneo hayo," alisema Mhandisi Sanda.

Mradi huo wa usambazaji maji katika wilaya za Musoma na Butiama ulisainiwa Novemba 17, 2021 mpaka sasa una zaidi ya miaka miwili, bado haujakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.


Aidha baadhi ya wananchi wilayani hapa waliomba serikali kufanya haraka kuwafikishia huduma ya maji ili kuwasaidia katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi na kukabiliana na adha ya ukosefu wa maji safi na salama.

Katika hatua nyingine, Mtanda alikagua ujenzi wa jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama, jengo la Jeshi la Uhamiaji, jengo la polisi na Hospitali ya Wilaya ya Butiama, akiwataka wahandisi kuacha tatizo la ucheleweshwaji wa miradi ya maendeleo bila sababu za msingi.



Ukurasa 14

Vita Israel inavyosambaratisha Gaza, nayo ikiangukiwa janga la kiuchumi




Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA FEBRUARI 23, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Ilipo tafsiri ya safari zake Samia na ukuaji wa diplomasia Uchumi

## • Tanzania, India kuuziana bidhaa kwa shilingi...

**Na Mwandishi Wetu**

MOJA ya wasifu mkuu anasimama nao Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nchini na kimataifa, kwamba amekuwa muumini wa vitendo wa diplomasia uchumi.

Kila baada ya muda, amekuwa akizunguka kimataifa akinadi uchumi wa nchi kimataifa, hali kadhalika akifungua soko la yapatikanayo nchini.

Hapo Rais Dk Samia ana sura kuu tatu; kuuza bidhaa na huduma nyingi nchini, zikiwamo kilimo na utalii; kukaribisha wawekezaji nchini katika sekta mbalimbali; na zao la yote inafungua wigo mpana wa ajira kitaifa.

Inaporejewa dhana pana ya diplomasia uchumi ambako Rais Dk. Samia ni muumini wake mkubwa, ina mzizi katika Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje, toleo la mwaka 2001, inayobeba tafsiri ya dhana ya "diplomasia ya uchumi."

Hapo inataja, mbali na malengo yake ya msingi kama vile kiulinzi, pia inajikita katika kujenga na kuimarisha uchumi wetu, inaushukilia uchumi wa nchi kiamtaifa, kwa wigo wa msimamo nchini.

Utekelezaji wa sera hiyo unaanzia katika kuimarisha misingi na umuhimu wa sera za asili za nchi, huku ikiongozwa na kanuni kadhaa, ikiwamo ya kulinda uhuru wa taifa, haki za binadamu, na usawa na demokrasia.

Kuna mengi yanaangukia zao la sura hiyo, ikiwamo kumkaribisha nchini Rais wa Romania, Klaus Iohannis, ambayo nayo ikajenga historia, kwamba kiongozi wa juu wa taifa hilo kutembelea Tanzania, hata ikasaidia kuimarisha ushirikiano katika maeneno ya kimkakati.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na mgeni wake, Rais wa Romania, Klaus Iohannis, alipowasili Ikulu jijini Dar es Salaam, Novemba, mwaka jana. **PICHA: MAKTABA.**

Rais Iohannis alifanya ziara ya kwanza ya siku nne na akaeleza kuwa, katika mazungumzo na mgeni wake walikubaliana kuwa mataifa yatakayoimarisha ushirikiano katika sekta za afya, hususan utengenezaji dawa, usindikaji mazao ya kilimo, madini na mbinu za kukabiliana na majanga.

Maeneo mengine ya ushirikiano ambayo viongozi hao wakadhamiria kuyapa kipaumbele, ni ufadhili wa masomo ambao Romania ikatoa nafasi 10 kwa ajili ya Watanzania kusoma masomo ya udaktari na ufamasia katika mwaka wa masomo uliopo.

Hapo, Tanzania nayo ikatoa nafasi tano za masomo kwa wanafunzi wa Romania kuja nchini katika vyuo watakavyochagua wenyewe, huku Dk. Samia akitangaza kudhamiria kukuza kiwango cha biashara na uwekezaji, nchini.

Rais wa Romania, Klaus Iohannis alikutana na kuzungumza na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi., aliyezikaribisha kampuni za Romania kuwekeza Zanzibar katika sekta za Uchumi wa Buluu na Utalii, ambazo ni sekta za kipaumbele huko Visiwani.

Hapo Rais Iohannis, akaeleza kufurahishwa na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar, akimuahidi Dk. Mwinyi, atashirikiana na Zanzibar kufanikisha utekelezaji wa dira hiyo.

Akasema ziara yake ni moja ya jitihada za kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, kati ya Romania na Tanzania, ambayo mwezi Mei 2024 utafikisha miaka 60 tangu ulipoanzishwa mwaka 1964.

Hadi sasa, Romania imeshaahidi kuisaidia Tanzania katika usindikaji wa mazao ya kilimo, nchini kukinufaika na teknolojia za kisasa ikisindika mazao ya kilimo na kuuza bidhaa nje badala ya malighafi, hata kimasoko inafungulia uingizwaji fedha za kigeni nchini kwa wingi.

Hati zilizotiwa saini Novemba 17, 2023 jijini Dar es Salaam, zikahusu ushirikiano wa kiuchumi, kisayansi na kiufundi katika sekta za kilimo na mazingira.

Mwanzoni mwa mwaka huo, mwezi Machi katika sura ya ushirikiano na taifa la India, ilifungua wigo kufanyika biashara ya mabadilishano yenye thamani ya shilingi trilioni 10.4.

Hapo ikawa ni kuingiza nchini bidhaa za India thamani ya shilingi trilioni 5.3 na Watanzania nao wakiuza nje bidhaa zenye thamani ya shilingi trilioni 5.1.

Kilicholeta mvuto mkubwa kitaifa ni namna biashara hiyo ikaafikiwa kufanyika, ambayo badala ya kutumika Dola za Marekani, sasa inatumika shilingi za nchini na Rupia ya India.

UCHUMI

# Uwekezaji madini ulivyopandisha daraja Kahama kwa uwanja ndege kupanuliwa

• Wachimba dhahabu wawekeza mabilioni; mgodini kuna ajira 3,000

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

TANZANIA kiuchumi inajulikana kuwa na utajiri wa madini, unaingizia kipato kwa asilimia kubwa, pia ajira kwa wananchi wake.

Hapo inajumuisha dhababu, almasi, shaba, nikel, chuma, magadi soda, makaa ya Mawe na vito mbalimbali kama tanzanite. Kulingana na hazina iliyopo, bado utafiti unaendelea kufanyika katika maeneo mengine kupata uhalisi wa utajiri huo.

Katika wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, kuna eneo lenye rasilimali ya madini ya dhahabu, asilimia kubwa ya wakazi wake wakijishughulisha na uchimbaji na uchakataji mdogo wa madini ya dhahabu na wanajiingizia kipato cha kuendesha familia, mbali na migodi mikubwa miwili ya Barrick Buzungwa na Bulyanhulu.

Mgodi wa Barrick Buzwagi, ndio kuna uwekezaji mkubwa na kuzalisha zaidi ya ajira 3,000 kwa vijana wa ndani na nje ya Shinyanga.

Namna ya uwekezaji mkubwa, kimuundo wa utendaji haujasahau kuhudumia jamii inayozunguka kupitia sekta mbalimbali za afya, elimu, maji, miundombinu ya barabara, kilimo na sasa inakabidhi jengo la Uwanja wa Ndege Kahama.

Dk. Mark Bristow, Rais na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick Duniani, wakati wa kukabidhi jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wilaya ya Kahama, uliojengwa na mgodi huo, kwa kushirikiana na Mamkala ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), akatioa ufafanuzi wa namna wanavyowajibika kwa umma.

Anasema jukumu lao liko endelevu, hawaishii uchimbaji madini pekee, wanatengeneza thamani kwa wadau wakati uliopo kuhakikisha kuwa kunaachwa urithi bora na endelevu, kuhudumia jamii kwa muda mrefu.

Dk. Bristow anasema, mgodi wa Buzwagi umedumu kitovu cha uchumi wa mkoa wa Shinyanga kwa takribani miaka 15 na ulikuwa mgodi wa pili kwa ukubwa nchini, ukiiajiri zaidi ya watu 3,000.

Hivyo, anasema wanaacha alama kwa kujenga miradi ya kimkakati kupitia madini yaliyokuwa yakipatikana.

Dk. Bristow anasema, maisha yake ya uendeshaji yalifikia tamati Julai 2021 na mgodi huo ulifungwa rasmi Julai 2022 na tangu wakati huo, Barrick imekuwa ikishughulikia ukarabati wa mazingira wa Buzwagi, huku pia ikiendeleza mipango yake ya kuubadilisha mgodi huo kuwa ukanda maalumu wa kiuchumi.



Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati) akikata utepe kuzindua jengo la abiria la Uwanja wa Ndege Kahama. Kushoto kwake Dk. Mark Bristow, Rais na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick Duniani. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi. Prof. Godius Kahyarara akifuatiwa na Mkuu wa Wilaya Kahama, Mboni Mhita. **PICHA: SHABAN NJIA**

Anasema, upembuzi yakinifu uliofanywa mwaka 2021 ulionyesha kuwa uundaji wa ukanda wa kiuchumi ulikuwa na uwezo wa kuchukua nafasi ya mgodi kama kichocheo cha uchumi wa mkoa huo.

Mtarajio yakawa uwezo wa kuzalisha ajira 3,000 kila mwaka na kuzalisha pato la zaidi ya Dola za Marekani Miliioni 150,000 (Bn. 38.250) kila mwaka kutokana na ushuru wa huduma kwa manispaa ya eneo.

**JENGO LA ABIRIA**

Dk. Bristow anasema, jengo la abiria limejengwa na Buzwagi kupitia mapato yaliyopatikana baada ya kuuza madini ya dhahabu kwa kushirikiana na serikali ni moja ya makabidhiano ya uwanja wa ndege waliokuwa wakiutumia katika shughuli zao na utafungua fursa za kiuchumi kwa watumiaji.

Anasema, Sh. milioni 896.7 zimetumika kujenga jengo hilo na kati ya hizo, Sh. milioni 615.8 zimetolewa na Barrick Buzwagi na Sh. Milioni 256.7 zimetolewa na serikali kupitia Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania (TAA).

Hapo anaishauri serikali kuboresha njia ya kuruka ndege kuwa ya lami, ili kipindi cha mvua ndege ziweze kushuka pasipo shida.

Dk. Bristow anasema jengo limejengwa na kampuni mzawa ya wilayani Mpanda, kazo iliyoanza Machi Mosi mwaka jana na kukamilika Novemba 30 mwaka huo, likiwa na uwezo wa kuhudumia abiria zaidi ya 200 kwa wakati mmoja, kulinganisha na jengo la awali lililokuwa likihudumia abiria 25 pekee.

**RC SHINYANGA & MBUNGE;**

Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anachukua nafasi hiyo kuipongeza kampuni ya Barrick, kwa kutumia sehemu ya mapato yake kujenga jengo la kisasa la abiria hapo, sasa akihimzia litunzwe kubaki kumbukumbu ya mgodi tajwa na kilichofanya, baada ya kufunga uzalishaji.

Mndeme anamuomba Rais Dk. Bristow, kutuma timu yake kwenda kutafiti madini wilayani Kishapu, wakifanikiwa waendeleze uchimbaji wa madini, kwani mkoa shinyanga una maeneo makubwa yenye madini na yanahitaji utafiti, wakiyabaini wachimbe na vijana waendelee kupata ajira.

Mbunge wa Kahama Jumanne Kishimba, anasema, kwenye ripoti ya ufungaji, ilifahamisha ardhini kuna madini mengi, ambayo kuyafikia yanahitaji gharama kubwa. Hapo anawasihi wasiyafukie mashimo hayo, ili bei ya dhahabu itakapopanda katika soko la dunia, basi wayachimbe tena.

**MKURUGENZI TAA/UCHUKUZI**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya viwanja wa Ndege Tanzania, Hamis Amiri anasema, jengo hilo litakuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 kulinganisha na jengo la awali linalobeba abiria 25 pekee na sasa wanajiandaa kujenga eneo la maegesho ya magari, thamani za ndani, Mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano hama, mifumo ya ufuatiliaji usalama la uwanja, mitambo ya kisasa ya kukagua abiria na mizigo.

Profesa Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, naye anasema kuwapo jengo hilo, kumeufanya Uwanja wa Ndege Kahama kupanda hadhi kufika Daraja la Tatu C (3C), akiahdi kuongezwa njia za kurukia kutoka kilomita 1.5, hadi kilometa mbili, ili kuhakikisha ndege za abiri9a zinafika hapo.

Anasema, serikali inaendelea kuboresha viwanja vya ndege ujenzi ukiendelea katika mkoa ya Mara, Tanga, Tabora, Arusha na Rukwa. Pia, anasema wilaya Kahama ikiwa karibu na nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Sudan Kusini na Jamhuru ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), basi uchumi naop utaongezeka, pia maendeleo yake kwa wananchi.

**MKAZI & ABIRIA**

Mkazi mkulima wa Halmashauri ya Manispaa Kahama, Ester Mabula anasema mgodi huo umewafanyia makubwa hasa kwenye sekta ya afya na kilimo, ikiujengea vituo vya kuongeza thamani na mazao yao, kisha watayasafirisha kwa kutumia kiwanja hicho, wakijiingizia kipato.

# AWAMU SITA INAVYOTUMIA ELIMU KUSUKA MAENDELEO

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA mikakati ya maendeleo kitaifa, serikali tangu uhuru imekuwa ikiwekeza kwenye huduma muhimu za jamii, ikiamini penye maboresho yake kunajenga msisimiko sahihi kiuchumi.

Sura ya huduma hizo zinajumuisha elimu, afya, makazi na nyenzo bora zinazowezesha roho ya nchi kiuchumi, sekta ya kilimo. Hilo katika awamu zote sita za uongozi nchini, hazijawahi kuachwa, bali zinabadilika kulingana na mahitaji ya wakati.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan naye katika zama zake madarakani, akiwa na sura ya maboresho ya ubunifu wake, anaendeleza, ikiwamo katika sekta yake kipenzi - elimu, ambako yu muumini hasa.

Hiyo inashuhudiwa hata na watendaji wake wateule, akiwamo Kanali Wilson Sakulo, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, katika ufunguzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Omom Preci iliyopo Loliondo, anapowaasa wananchi kijijini na kata ya Enguserosambu, kuhakikisha hawakai mbali na sera, pia falsafa ya Ukombozi wa Elimu kwa kila Mtanzania.

Msaidizi huyo wa Rais Nambari Moja, wilayani hapo, anawakilisha wasifu wake kuwa sauti na kioo cha serikali kinachosisitiza elimu kwa wote.

Katika hafla hiyo hivi karibuni, kamanda huyo anaawaambia umati wilayani kwake kuwa, Rais Dk. Samia na serikali ya Awamu ya Sita tangu alipochukua Madaraka, vitendo na maneno yake vimeonakana kuhimzia elimu.

Hivyo, Kanali Sakulo anawataka wananchi hao kutokuwa na visingizio mbadala dhidi ya 'elimu bure shuleni' kwa watoto wao, utekelezaji wake ukifikishwa kwa kila mwananchi alipo nchini.

Kimsingi, kwa miaka mitatu, Rais Dk. Samia tangu ashike madaraka Machi mwaka 2021, amedumu kuwa muumini wa kupatikana elimu kwa watoto wote wa Kitanzania, akikataa mzaha dhodi yake.

Huo umedumu kuwa mwelekeo na falsafa inayoendelezwa na wasaidizi wake kikazi, kwa ngazi mbalimbali kama vile; Wakurugenzi wa Halmashauri (DED s), maofisa wanaowasaidia, pia watunga sera za elimu ngazi mbalimbali, wakizama katika imani na itifaki hizo kikazi, ambayo pia ndio uhai wa nchi.

Eneo moja la mfano katika hatua zake Rais Dk. Samia, akaanza kutumikia wajibu wa ukuu wa nchi kama mama mwaka 2021, kwa kuwarudisha shuleni wanafunzi wanaopata mimba.

Hapo ndipo Mkuu wa Wilaya Kanali Sakulo, akiwaambia wananchi wake kuwa hakuna kisingizio chochote kukaa mbali na shule katika Serikali ya Awamu ya Sita.

Kihistoria, elimu ni kigezo muhimu sana katka kuleta maendeleo ya nchi, hivyo serikali zianwajibibika kuwasimamia na kuwanasua wanapokwama katika safari ya raia kuelekea kuelimika.

Ndipo kunashuhudiwa udhamini wa serikali masomoni na sheria chanya, kusaidia wanaosoma. Itakumbukwa ndilo alilifanya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, mara tu alipokabidhiwa dhamana ya kuongoza nchi, baada ya uhuru.

Suala la elimu nchini linasisitizwa kila mara na kila, mahali kifalsafa na kimatendo ikiendelezwa sasa serikalini katika staili hata aliyeachwa nyuma anakokotwa kufika safari.

Nchini kuna matukio ya mazoea na mila, baadhi ya wana wanafunzi kuozeshwa au kuolewa kutokana na kukosa nafasi ya pili ya kurekebisha makosa yao.

Hapo ndipo Serikali ya Awamu ya Sita, inatumia kigezo maendeleo, ikitumia elimu kuwa 'ufunguo wa maisha' kwa wahusika, mahsusi kwa watoto wa Kitanzania.

Inafahamika, maeneo ya mijini na vijijini, kunawanafunzi wanaopata mimba za utotoni. Pasipo kujali takwimu, suala la mimba hizo limekuwa nyeti, kwani linadhoofisha maendeleo ya watoto husika.

Kwa kutambua kuwa taifa linaweza kuangamia kwa kuruhusu wanafunzi waliopata mimba, wakikosa fursa za elimu tena, serikali sasa imekuja na mpango unaonufaisha wananchi na kuwaondolea kero ya kukoda elimu.

Pili, kinachoshudiwa, Rais Dk. Samia amefanya ubinfu, akituimia pia wahisani kupata mikopo na ufadhili za kuzibna mapengo kwenye uwezeshaji sekta elimu.

Miongoni mwa miradi iliyookoa sekta ya elimu ni pamoja na ufadhili wa fedha za kufharamia tiba Uviko 19, sasa zikahamishiwa kujenga vyumba vya madarasa sehemu mbalimbali nchini.

Katika marejeo ya suala la ujenzi wa vyumba vya madarasa, limepata kukumbushwa pia wakati wa uzinduzi wa Omom Preci inayofadhiliwa na Shirika la Tanzania Heritage Foundation, ambako Mkuu wa Wilaya Ngorongoro, anayesisitiza wananchi kupewa nafasi ya kupata elimu kutoka kwa watu binafsi na serikalini.

Hapo, wananchi wanatakiwa kutumia fursa hizo, kwani serikali inawapa nafasi wadau kuchangia.

Fedha hizo pia zilitumika kutengeneza madawati ambayo yamekuwa msaada kwa wanafunzi na kutatua kero yao sehemu mbalimbali.

Ni aina ya juhudi zinazoifanya serikali ya sasa, kubeba sifa za ukombozi thabiti wa elimu na kupigania ustawi wa jamii, katika safari ya kuyasaka maendeleo.

Lingine linalotajwa, linasimama katika kinachohimizwa na Rais, mkakati wa serikali kumiliki shule za msingi na sekondari zenye mkondo wa lugha ya Kiingereza.

Tayari zipo shule za serikali zinafundisha kwa kutumia mkondo wa lugha ya Kiingereza na kuwapo mtaala mpya unaokaribisha somo la Kichina, ambalo sasa ni sehemu ya stadi za Uchumi na maendeleo ya dunia.

Hiyo pia, ni mustakabali unaowapa nafasi wadau binafsi na watumishi watoto wao wanapata elimu sahihi, vilevile katika sura ya pili taifa nalo likijiboresha mahitaji yake kitaifa na kimataifa kwa; biashara, kiuchumi, kijamii na mawasiliano.

Hapo napo panapandisha thamani ya shule za serikali na elimu ya nchj kimataifa, kukiwekwa jicho kali elimu bora kuwa na sura endelevu.

Hapana shaka, wakati serikali ya Awamu ay Sita, moja ya mitaji yake ya mipango elimu, kunashuhudiwa sekta ya elimu ambako hata ngazi ya juu vyuoni, kumekuwapo maboresho ya mikopo hadfi ngazi za chini, upendeleo wa kijinsia, udhamini wa masomo.

Pia, wiki hii kumetangazwa mwelekeo ya kusuka upya mtaala wa Shule ya Sheria, inayozalisha watalamau wa mahakamani, ambako ni nguzi kuu ya dola, sambamba na bunge, pia serikali.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tunaiga mambo ya wageni mpaka hatua inachukiza

ZAMANI wakati tunakua, tulikuwa tukiwasikia wazee wetu wakituonya dhidi ya baadhi ya tabia, huku wakituhadharisha kuwa ni mbaya, kwani zinafanywa tu na Wazungu na si utamaduni wetu.




Mara nyingi wakiona wasichana na wavulana wakibusiana hadharani, au wasichana wakivalia nguo fupi zikiwamo sketi, waliwaonya na kuwakaripia, kuacha kuiga tabia hizo potofu za kigeni.

Lakini ni bahati mbaya, kwamba vijana waliona kila kilichofanywa na Mzungu bado kilikuwa cha kistaarabu, huku wakibeza walichokifanya wao na kukiona kuwa ni ushamba.

Ndiyo sababu hata wasichana wakawa wanavaa mawigi wakati huo sisi tukiita ni 'Nywele za Maiti wa Ulaya' na kwingineko ughaibuni. Lakini, hakuna aliyeshituka akiona ni bora kuvaa nywele hizo kuliko kukaa na kipilipili.

Wavulana nao wakichana au kunyoa nywele na kuweka wei, ili kuonekana kama walivyokuwa wakionekana Wazungu, ingawa wao nywele zao zikilazimika kuwa na wei kutokana na maumbile na si kunyoa.

Kasumba hiyo iliendelea mpaka pale wasichana walipojikuta, pia wakibandika kucha ndefu kama walivyofanya Wazungu na wakati mwingine tunakumbuka kuna waliochonga pua zionekane mchongoko kama za Wazungu.

Tukaendelea kuishi hivyo, mpaka tukafikia hatua ya kudharau lugha zetu za makabila, hata kwa Taifa na kuamini kwamba bila kuzungumza Kiingereza mtu hajastaarabika. Sijui ndiyo sababu Mswahili akilewa huzungumza Kiingereza kuonekana mstaarabu?

Tabia hiyo ilifikia hatua hata kuamini kwamba, kumbe tukikosa hata mavazi, basi ni bora kuagiza nguo zilizokataliwa au kuachwa na Wazungu, tukiziita 'Kafa Ulaya' na sasa ina jina mitumba.

Tukaacha hata pia kula maharage ya nchini na kutamani kula ya ughaibuni, licha ya kuwa na ardhi nzuri na ya kutosha kuzalisha mazao ya chakula ya kututosheleza.

Pia, jamii ilijitahidi kukemea tabia kama hizi, lakini hivi sasa tunaona hakuna anayeelewa kabisa baada ya kuona kuwa kumbe maendeleo hutoka Ulaya na hivyo hata matibabu tukaona bila kutibiwa ughaibuni mtu hajapona.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

Hivi sasa kuna mambo ya mapya ya aina yake kabisa, watu wamefikia hatua ya kurekebisha maumbile kwa kuwa tu nao ni Wazungu na wanafanya hivyo, ili kuvutia wengi na wanaofanya hivyo ni wasichana au

Wanawake, wanaoongeza ukubwa wa maumbile yao.

Umefika wakati hilo loinagfanyika katika hosopiuali kubwa hasa nchini, watu wanakaribishwa kufanya marekebisho hayo yanayoshajiishwa na madaktari, ili wanawake hao wavutie kimaumbile.

Kwangu naona mwelekeo mkubwa unapaswa kuangukia kuwekezwa kwenye matibabu ya magonjwa yanayoigubika jamii. Sidhani kipaumbele ni kuzama kubadilisha maumbile ya wanawake! Au ni biashara mpya?

Niseme, kama tuna madaktari wa aina hiyo nchini na vifaa vya aina hiyo, kwanini wasipelekwe au vifaa tiba hivyo visipelekwe hospitali ya kurekebisha viungo ya CCBRT, ambako wenye ulemavu wamekuwa wakifanyiwa tiba za kurekebisha viungo?

Ni jambo lenye tija, kuona madaktari wetu wanafanya marekebisho kwenye viungo vya waliozaliwa wakiwa na ulemavu wa viungo au waliopatwa na ajali, kuliko kuendekeza watu wanaotafuta urembo.

Inashangaza, leo kuona msichana eti anajibadilisha hata sura na rangi, ili mradi aonekane mweupe na kufanana na Mzungu huku akiwa amezaliwa na wazazi wake wenye rangi nyeusi halisi na nzuri ya Kiafrika.

Tunaendelea kuiga uzungu, ambao hivi sasa tunasikia kuna kingine kinanipa tabu kusikia kunazishwa utaratibu hospitalini wa wazazi wa kiume, kwenda kushuhudia wenza wao wakijifungua! Ina tija gani hii?

Hivi nani amefanya utafiti na kubaini kuwa mwanamke akijifungua huku akishuhudiwa na mumewe uchungu hupungua, au mtoto huzaliwa salama, kuliko anapokuwa mwenyewe na msaada wa wauguzi?

Yote yanaingia kwenye kasumba za wezetu wa magharibi, kuiga mambo ambayo hayana hata faida na umuhimu kwa jamii, kama ambavyo polepole tunaingizwa kwenye imani za ushoga na kusababisha wenzetu kuingia huko na kupotoka.

Tukiuliza, tunajibiwa kuwa ni usasa na utandawazi miongoni mwa jamii, hivyo kufananafanana na Wazungu, ambao kwa bahati mbaya sana, tunaendelea kuwaamini kwamba kwa kuwa wametuzidi kwa mengi, basi tumeze kila kilicho chao.

Kama alivyopata kusema Hayati Rais John Magufuli enzi zake, tusipoangalia na kujikuta tumeingia katika kuiga mambo kama hayo yasiyo na maana, basi tutakuwa na haki makaburi yetu kuchapwa viboko.

Hiyo inatokana na kudharau nafsi zetu, kushindwa kulinda, hata kutetea utamaduni wetu na badala yake kujishushia hadhi. Bora kujiuliza kwanini hatusikii Wazungu wakiiga ya kwetu?

Tunajitoa akili wenyewe! Mungu endelea kutusaidia.

UCHUMI

# Vita Israel inavyosambaratisha Gaza, nayo ikiangukiwa janga la kiuchumi

## • Viwanda vyafungwa, ubinafsishaji ghafla
## • Makadirio ya ukuaji uchumi yabomoka



Wakazi wa Israel wakitoka kununua bidhaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kila siku ya nyumbani. **PICHA MTANDAO.**

**Na Maulid Mmbaga**

VITA vya Israel dhidi ya Wapalestina wenye makazi katika ukanda wa Gaza, sasa vimeingia mwezi wa nne, si kwamba tu imeishia kusambaratisha Palestina kwa sura pana.

Hapo inajumuisha, kuuawa raia wake 28,000 mpaka sasa, pia kwa Israel nayo inaachwa katika kilio ikiwamo cha kiuchumi.

Kuna athari kubwa kwa uchumi kwa Israel ikisababisha viwanda vyake vingi kusimamisha biashara, vichache vikiendelea kupata uwekezaji mpya kwa kufanyiwa ubinafsishaji.

Inaelezwa kuwa tangu Oktoba 7, 2023, Hamas ilipoivamia Israel, serikali ya taifa hilo imetoa ruzuku ya mishahara ya askari wa akiba 360,000 waliotumwa Gaza, ambao wengi wao ni wafanyakazi katika masuala ya fedha, akili bandia, dawa na kilimo.

Inabainishwa kuwa Novemba mwaka jana, Benki ya Israel iliweka bayana athari za vita hivyo katika taifa hilo, ikiwamo kuingia gharama ya dola bilioni 53 (Sh. Trilioni 134.3) hali iliyorudisha nyuma makadirio yake ya ukuaji uchumi kwa asilimia mbili kwa mwaka fedha uliopo- 2023/24, uliotarajiwa kukua kutoka asilimia 2.3 hadi asilimia 2.8.

Disemba iliyopita, Wizara ya Fedha ya Israel ilieleza kwamba vita hivyo vitagharimu pia Israel takriban dola bolioni 13.8 (Sh. Trillion 35) mwaka huu, ikiwa awamu yake ya hali ya juu itakamilika katika robo ya kwanza ya mwaka huu.

### HALI YA WASIWASI

Mwenyekiti wa Kituo cha Mafunzo ya Sera za Kijamii kipalestina, Benjamin Benntal, anasema maofisa wa Israel wanakabiliwa na changamoto ya kuhitaji kurejesha imani na hali ya usalama ambayo haitakuwa rahisi kukuza uwekezaji.

"Zaidi ya matokeo ya wazi ya kijeshi na kisiasa katika Ukanda wa Gaza na kwenye mpaka wa Lebanon, na kuwarejesha nyumbani mateka, hii inahitaji sera ya kiuchumi iliyo wazi na yenye malengo. Bado haijabainika jinsi gani hili litashughulikiwa," anasema Bental.

Inabainishwa kuwa, nchini Israel migahawa na maduka inaendelea kubaki tupu baada ya Hamas kuivamia na kusababisha vita huko Gaza, na kwamba orodha ndefu ya mashirika ya ndege ilighairi au kusitisha safari zao nyingi za ndege kwenda mji mkuu Tel Aviv, na watalii wengi walighairi mipango yao ya kutembelea taifa hilo.

Inaelezwa kuwa kabla ya operesheni ya Al Aqsa, wageni waliotembelea Israel walikuwa zaidi ya 300,000 kila mwezi, huku Novemba, 2023 idadi hiyo ikiripotiwa kupungua hadi 39,000.

### MIRADI YASIMAMISHWA

Ujenzi nao unaochukua asilimia 14 ya pato la taifa la Israel, inatajwa kuangukia pigo kubwa tangu vita hivyo vianze na kusababisha miradi ya ujenzi kusitishwa na Israel kwa muda usiojulikana tangu Oktoba 2023.

Inaelezwa kwamba ilizuia vibali vya wafanyakazi kwa Wapalestina ambao ni asilimia 65 hadi 70 ya wafanyikazi katika sekta ya ujenzi nchini humo.

Inaelezwa kuwa, sekta hiyo na uchumi katika Ukingo wa Magharibi umepata pigo kubwa, kwa kuwa kati ya Wapalestina 110,000 waliokuwa na vibali vya kufanya kazi Israel, wengi wao walikuwa wakifanya kazi katika ujenzi.

Inabainishwa kuwa, pengo hilo halijazibwa na wafanyakazi wa Israel, kutokana na jinsi askari wa hakiba wameitwa kupigana vitani, huku wafanyakazi wa kigeni kwa wingi wakitaja kuikimbia Israel kutokana na mzozo huo.

Jumuiya ya Wajenzi wa Israel, nayo inasema nchi hiyo inapanga kuleta takriban wafanyakazi 70,000 wa ujenzi kutoka mataifa ya China, India, Moldova na Siri Lanka.

### UAGIZAJI BIDHAA

Kutokana na hali hiyo inaelezwa kuwa kwa sasa Israel inaagiza kutoka nje almasi, magari, mafuta ya petroli, na vifaa vya utangazaji na bidhaa mbalimbali kupitia Bahari Nyekundu.

Taarifa zinaeleza kuwa, ni hivi karibuni makombora ya Houthi na ndege zisizo na rubani zilizoshambulia meli za mizigo kama kulipiza kisasi shambulio la Israel huko Gaza, yamevuruga biashara ya kimataifa, na uagizaji wa bidhaa Israel. Inafafanuliwa, kwamba uagizaji mwingi wa nchi hiyo kutoka Asia sasa unaelekezwa barani Afrika, na hivyo kuongeza gharama maradufu.

Kuna maelezo kwamba, ni takriban asilimia 20 ya umma wa Waisraeli wanaripoti mapato ya kaya zao yameathiriwa kwa kiwango kikubwa, tangu kuanza kwa vita vya nchi yao dhidi ya Hamas huko Gaza.

Katika uchunguzi wa hivi majuzi, shirika la misaada la Latet, liligundua kuwa zaidi ya asilimia 45 ya wananchi wanahofia kwamba, matatizo ya kiuchumi yanawangoja baadaye, katika vita hivi au baada ya vita kumalizika.

Athari nyingine ya wazi ni kwamba familia hizo za Waisraeli tayari zilikuwa zikiishi katika umaskini au zilizohitimu kuwa na uhaba wa chakula kabla ya Oktoba mwaka jana, zitaathirika zaidi kutokana na matatizo ya kiuchumi yanayotokana na vita hivyo.

"Ni vigumu kujua nini kinaendelea katika mawazo ya wanasiasa wetu, lakini Waziri Mkuu Netanyahu na serikali yake wanakabiliwa na shinikizo la kidiplomasia la kimataifa, ambalo halijawahi kutokea ili kumaliza vita na uchumi wa vita hauna nafasi ndogo katika kufanya maamuzi," anasema Fuld.

### TEKNOLOJIA INAVYOWABEBA

Inafafanuliwa kuwa, licha ya biashara kutetereka, lakini moja ya sekta ambazo zimeendelea kufanya vizuri ni ya teknolojia ya hali ya juu, eneo lake linalokuwa kwa kasi zaidi kwa miaka kadhaa, ambalo kwa sasa linachukua karibu asilimia 20 ya pato la taifa (GDP) na asilimia 14 ya ajira.

Inabainishwa kuwa, Israel imejiimarisha kama kituo kikubwa zaidi cha teknolojia duniani, cha pili baada ya Silicon Valley. Na kwamba zaidi ya mashirika 500 ya kimataifa kutoka Google, Apple, IBM, Meta, Microsoft, Intel Corp hufanya kazi nchini Israel.

Inaelezwa, kutokana na Israel kujihusisha na vita huko Ukanda wa Gaza, kumekuwa na wasiwasi kwamba juu ya kampuni hizo kuendelea na uwekezaji wake katika taifa hilo.

### BIASHARA YA TEKNOLOJIA

Pia, kuna ufafanuzi kwamba ndani ya wiki moja baada ya Hamas kuishambulia Israel, athari ya mara moja ni zaidi ya kampuni 220 za mtaji, zilitia saini taarifa kueleza mshikamano wake na taifa hilo yakitoa wito kwa wawekezaji kuendelea kuunga mkono mfumo wake wa kiteknolojia, mbap inaufanyia biashara.

Kuanzia Disemba 17 hadi 20, 2023 watendaji wakuu kadhaa kutoka Marekani wa teknolojia walishiriki katika 'misheni' ya Israel Tech, iliyohusisha mikutano ya sekta ya teknolojia huko Jerusalem na Tel Aviv, kati ya watendaji hao na maofisa wakuu wa serikali ya Israel.

Ron Miasnik, ni mwekezaji na mshirika wa Israel katika sekta ya teknolojia, anasema akiwa muwekezaji wa muda mrefu katika mfumo wa ikolojia Israel, wamefanya kuwa kipaumbele kukutana na timu hiyo, ili kuelendea kusaidia utulivu wan a ustawi wa kiuchumi katika eneo hilo.

"Kwa muda mrefu, tunaamini katika uthabiti wa mfumo wa ikolojia wa uanzishaji wa Israel na tumejitolea sio tu kuendelea lakini kuongeza umakini wetu kwenye eneo hilo," anasema.





# RC amsimamisha kazi Mtendaji Kata tuhuma za ulevi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amemsimamisha kazi Mtendaji wa Kata ya Manchali wilayani Chamwino, Waitara Wambura kwa madai ya kulewa pombe wakati wa kazi.

Senyamule alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ya wilaya hiyo, kuagiza uchunguzi zaidi ufanyike wa utendaji kazi wake.

Hivyo alimuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, kufanya uchunguzi wa kina juu ya utendaji kazi wa mtendaji huyo ambaye ameonesha utovu wa nidhamu na kukiuka maadili ya kazi.

Pamoja na hayo, aliuagiza uongozi wa halmashauri hiyo kukamilisha ujenzi wa uzio wa ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kabla ya Machi 30, mwaka huu kutokana utekelezaji wake kusuasua tangu ulipotakiwa kukamilika Julai 2023. "Chamwino kwa sasa siyo nzuri, mkoa una halmashauri nane na katika halmashauri hii kila miradi inayokuja lazima zijitokeze changamoto, tunapokea malalamiko yenu mengi hasa suala la malipo kwa makandarasi wanaojenga miradi yenu," alisema Senyamule.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Godwin Gondwe aliahidi kusimamia miradi inayotekelezwa katika wilaya hiyo na kukamilika kwa ubora na muda uliopangwa.



Ofisa Elimu kata ya Chihanga Jiji la Dodoma, Christopher Mwatowine akipokea moja wa mifuko ya sukari ya kilo 25 iliyotolewa kwa ajili ya matumizi ya shule kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri ( wa pili kulia) wengine ni Mstahiki Meya Jiji la Dodoma Prof. Davis Mwamfupe, (kulia), Kaimu Mkurugenzi Jiji, Joseph Fungo, (wa pili kushoto) na Katibu Tawala Wilaya Sakina Mbugi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# LAAC yaipongeza TAMISEMI kuanzisha ufundishaji mubashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeipongeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kuja na mfumo wa ufundishaji mubashara ambao utasaidia kukabiliana na upungufu wa walimu nchini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Halima Mdee alitoa kauli hiyo wakati wa ziara ya LAAC ilipofanya ziara ya kuona namna matumizi ya mfumo huo unavyofanya kazi katika Shule ya Sekondari Dodoma.

Alisema hatua ya kuja na mfumo huo umekuja wakati muafaka ili kukabiliana na upungufu ambao kwasasa takribani walimu 270,000 wanahitajika.

"Kuajiri n i jambo moja na kuwa na uwezo wa kulipa mishahara kutokana na hali ya uchumi na uwezo wa nchi ni jambo lingine, wakati nchi inapojipanga kuweza kuajiri watu wengi lazima tuangalie watoto wetu katika hali ya sasa tunashughulika nao vipi, kwa hiyo ni mfumo ambao umekuja wakati sahihi,"alisema.

Mdee alisema kuwapo kwa mfumo huo ni suluhu ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kutokana na sasa kuwa dunia ni ya kidijitali na kuwa wao kama wabunge watasaidia katika kusukuma suala hilo ili serikali iltekeleze nchi nzima.

Mdee alishauri pia Kamati ya Bunge ya Bajeti iuone mradi huo ili kuwe na msukumo wa kuutengea bajeti katika siku zijazo.

Hivi karibuni, akizindua mfumo huo, Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, alisema mfumo huo unamuwezesha mwalimu mmoja wa sayansi kufundisha wanafunzi wa nchi nzima kwa wakati mmoja.

Kutokana na hilo, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri wameagizwa kutenga katika bajeti ya mwaka 2024/25 fedha za kutosha za kununua vifaa vya TEHAMA.

Alibainisha kuwa kwa upande wa elimu ya awali na msingi uhaba ni walimu 186,385 na kwa sekondari ni 84,643.

# PSSSF yapewa siku 100 kukamilisha ujenzi wa kiwanda

**Na Mwandishi wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, mhandisi Cyprian Luhemeja ametoa siku 100 kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Wafanyakazi wa Umma (PSSSF), Abdul-Razaq Badru kuhakikisha awamu ya pili ujenzi wa kiwanda cha kuchakata bidhaa za ngozi Kilimanjaro unakamilika na kuanza kufanya kazi ifikapo Julai 2024.

Alilitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kukagua ujenzi katika kiwanda cha bidhaa za ngozi Kilimanjaro (KLICL) ikiwa ni sehemu ya kukagua maendeleo ya miradi inayotekelezwa na serikali kupitia ofisi hiyo.

Luhemeja alisema kukamilika kwa kiwanda hicho kutaongeza thamani ya zao la ngozi ghafi, kufungua fursa za soko la uhakika la ngozi kutoka kwa wafugaji, kuongeza ajira kwa vijana na mapato ya fedha za ndani na za kigeni.

Aidha, alifurahishwa na ubora wa bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo na kutoa wito kwa Watanzania kuwa na utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazo zalishwa nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru alisema amepokea maagizo hayo na kuahidi kuwa PSSSF kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza watahakikisha wanafanya kazi kwa weledi kama ilivyoelekezwa ili Watanzania waanze kunufaika na mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Saiba Edward alisema mradi huo pamoja na mambo mengine utaongeza kipato kwa wakazi wa Kilimanjaro na mikoa jirani kupitia fursa za uzabuni, uwakala na usambazaji wa bidhaa.

Kamishina Msaidizi wa Jeshi la Magereza, Frank Mwakijungu alibainisha kuwa Magereza ni mbia wa utekelezaji wa mradi huo, hivyo watasimamia ujenzi wa kiwanda hicho ili kikamilike kwa wakati kwa manufaa ya Watanzania.

# RC aipa mtihani TARURA usimamizi miradi ya ujenzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba ameiagiza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) kusimamia miradi yote ya ujenzi na matengenezo ya barabara, ikamilike kwa wakati.

Serukamba alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja inayoendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Iramba na Mkalama.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kuiunganisha miji kwa lami, hivyo ni wajibu wa viongozi wote kushirikiana kuisimamia ijengwe vizuri ili ilingane na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali.

Serukamba pia aliiagiza TARURA kuomba fedha serikalini kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Mto Ntwike kwani Barabara ya Meli-Walla hadi Ntwike inayojengwa hata itakapokamilika haitakuwa na maana kama daraja halitajengwa.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Iramba, Evance Kibona, akitoa taarifa ya ujenzi wa miradi alisema wilaya hiyo imetengewa Sh. bilioni 6.836 ambazo chanzo chake ni kutoka katika Mfuko wa Barabara, ushuru wa mafuta na katika mfuko wa serikali.

Kibona alisema hadi kufikia Januari 2024 Sh.bilioni 1.922 zimepokelewa ikiwa ni sawa na asilimia 28 ya Sh.bilioni 6.836 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara katika wilaya hiyo.

Kaimu Meneja TARURA Wilaya ya Mkalama, Mhandisi Paschal Mafuru, alisema wilaya hiyo imetengewa Sh.bilioni 2.513 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja.

Alisema hadi kufikia Januari 30, 2024, Sh.milioni 727.803 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 29 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kazi za ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Ibrahimu Kibasa alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kwamba miradi hiyo inayotekelezwa TARURA itaendelea kusimamia makandarasi waliopewa zabuni ili iweze kukamilika kwa wakati kukingana na mikataba inavyoelekeza.





## H/shauri yaanza kutoa fedha uendeshaji serikali za mitaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji Makambako mkoani Njombe, imeanza utaratibu wa kutoa Sh. 200,000 kwa ajili ya ofisi ya serikali ya mtaa, ili kusaidia uendeshaji na kuwaondolea adha wenyeviti kutumia fedha zao za mfukoni.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa katika kikao na wenyeviti wa serikali za vijiji na mitaa.

Mfikwa alisema fedha hizo zitatolewa kila baada miezi mitatu ili ofisi hizo ziweze kujiendesha bila ya kuwa na changamoto yeyote.

Mfikwa aliwataka wenyeviti hao kuwa wawazi katika maeneo yao kwa kuwasomea wananchi taarifa za mapato na matumizi pamoja na kutatua matatizo ya wananchi kwa wakati

"Wenyeviti wamejua wajibu wao ni nini wanapokuwa kwenye mitaa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanaitisha mikutano kwa wakati lakini wanawasomea wananchi mapato na matumizi pamoja na kuwa wawazi kwenye miradi yao," alisema Mfikwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Kenneth Haule aliwataka wenyeviti wa serikali za mitaa kutojihusisha na uuzaji wa ardhi ama kuingia mikataba na kampuni yanayotaka kuwekeza katika maeneo yao.

Nao baadhi ya wenyeviti akiwemo Mwenyekiti wa Mtaa wa Kisiwani, Rajabu Shayo alisema changamoto yao kubwa hapo awali ilikuwa ni kukosa fedha za uendeshaji wa ofisi na kueleza kuwa kwa sasa watafanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

"Mimi nimefurahi kwa sababu uendeshaji wa ofisi ulikuwa ugumu, ebu fikiria mtu ulikuwa huna hata kitu alafu nakuletea Sh. 200,000 baada ya miezi mitatu sisi shida ya zile fedha ilikuwa ni kuendeshea mitaa," alisema Shayo.

Aidha Mwenyekiti wa Mtaa wa Sigridi, Bahati Nyato aliishukuru halmashauri kwa kusikiliza malalamiko yao ambayo yameleta tija kwa sababu hapo awali walikuwa wakitoa fedha zao mfukoni kuendeshea ofisi.



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge ,Dk Tulia Ackson, akifurahia jambo na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera wakati walipokutana katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa huyo zilizopo Jijini Mbeya jana. **PICHA: BUNGE**

# 17% wajawazito Nyanda za Juu Kusini Magharibi wanajifungulia nyumbani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 17 ya wajawazito katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi wanajifungulia nyumbani badala ya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, hali ambayo inazorotesha huduma ya afya ya mama na mtoto.

Mtakwimu Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Elinzuu Nicodema aliyasema hayo juzi alipozungumza na wataalam wa afya wa mikoa mitano ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi wakati wa utoaji wa matokeo ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2022.

Kwa mujibu wa NBS, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi inaundwa na mikoa minne ambayo ni Mbeya, Rukwa, Songwe na Katavi lakini kwenye kikao hicho wataalamu wa afya kutoka Mkoa wa Njombe pia walishiriki.

Elinzuu alisema asilimia 90 ya wajawazito katika kanda hiyo wanahudhuria mahudhurio yote ya kliniki kwa ajili ya kupima maendeleo ya ujauzito lakini wakati wa kujifungua wengine hawaonekani kwenye vituo vya afya.

Alisema hata kwenye takwimu za kitaifa tatizo hilo ni kubwa na kwamba linatofautiana kati ya kanda na kanda na hivyo akawataka wataalam hao wa afya kusaidia kutoa elimu.

"Tatizo hili ni kubwa lakini linatofautiana, kuna maeneo mengine unakuta ni asilimia 15, 16, 17 mpaka 20, hii inatakiwa tufanye kazi kwa ushirikiano ili kupunguza tatizo hili, tumefanya vizuri kwenye mahudhurio ya kupima maendeleo ya ujauzito ambapo wajawazito wetu wanahudhuria mahudhurio yote manne ila kujifungua ndio shida," alisema Elinzuu. Hivyo, aliwataka wataalamu hao wa afya kuweka mikakati maalumu ya kukabiliana na tatizo hilo ili wajawazito wote wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Vilevile aliwaomba watafiti kufanya utafiti ili kubaini sababu za wanawake hao kujifungulia nyumbani na kushauri namna sahihi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Bonface Kasululu alisema takwimu zilizotolewa na NBS zitawasaidia kufanya tathimini na kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo na kwamba watahakikisha wanalimaliza.

Alisema pamoja na kwamba takwimu hizo zinaonyesha kwamba hali siyo nzuri lakini bado kuna mabadiliko makubwa kwa maelezo kuwa miaka ya nyuma hali ilikuwa sio nzuri.

Alisema hata takwimu za kitaifa zinaonyesha kwamba kuna mabadiliko kwa maelezo kuwa mpaka sasa asilimia 90 ya wanawake wanajifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Nyema alisema tatizo hilo la wajawazito kujifungulia nyumbani linasababisha kuendelea kuwepo kwa takwimu za vifo vya wajawazito na watoto wachanga na hivyo akasisitiza kuwa wana kazi kubwa ya kufanya.

Alisema: "Tunashukuru takwimu hizi zinaonyesha kwamba kuna maendeleo mazuri kwenye eneo hili tunatakiwa tushirikiane kuhakikisha tatizo hili linakwisha kabisa".

## Ukosefu soko la mananasi chanzo cha umaskini wakulima Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UKOSEFU wa soko la uhakika la mananasi yanayozalishwa katika Kijiji cha Madeke Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, limedaiwa kuwakatisha tamaa wakulima kuendelea na kilimo hicho, wakisema kinawasababishia umaskini na kushindwa kutoa huduma muhimu kwenye familia zao.

Wakulima hao walisema walijikita katika kilimo cha nanasi kwa lengo la kujiingizia kipato, lakini matokeo yake imekuwa tofauti baada ya kuzalisha nanasi na kukosa soko hali iliyowafanya kupata hasara.

Mkulima Grace Mbote alisema hali yao ya maisha ni ngumu kwa sababu kilimo cha mananasi ndiyo wanachokitegemea na wamelima kwa wingi lakini wamekosa masoko na kuomba serikali kuingilia kati na kutatua changamoto waliyonayo.

"Wenye mashamba wakulima wakubwa wanakuja na magari yao kutoka Njombe mjini na kubeba nanasi kwenda kuuza wanapojua wao isipokuwa siye wadogo tunakosa masoko ya uhakika, tunaomba serikali kuingilia kati na kututafutia soko kama wanavyofanya kwenye mazao mengine ya biashara," alisema Mbote.

Costantino Joram alisema changamoto ya kilimo cha manansi kijijini hapo ni kukosekana kwa soko.

"Hatuna soko na mashamba yametelekezwa, hatuna chombo cha kusafirishia mazao kwa sababu wakulima anatakiwa akavune alafu abebe kichwani alete barabarani jambo ambalo ni mateso," alisema Joram.

"Napo mteja akipatikana mnagombaniana, kama umepata mteja mzuri basi Sh. 300 kwa hiyo bei ya nanasi kwa ujumla siyo nzuri," alisema Joram.

Kwa upande wake, Jane Lianzi alisema kuwa zao la nanasi hapo mwanzo lilikuwa likiwanufaisha kiuchumi ikiwemo kuwasomesha watoto na kufanya kilimo kingine cha muda mfupi kama maharage.

"Kwenye nanasi kumeshakufa kiujumla kwa sababu inapofika Januari yanaanza kuoza hakuna mtu anayenunua kwa sababu hakuna pa kuuzia, lakini ilivyoonekana tumeshakufa kimfumo wa maisha, kusomesha watoto imeshakuwa ngumu na ukienda shambani kumebaki pori tu," alisema Lianzi.

Ofisa Kilimo Kata ya Mfriga, Onesmo Mfugale alikiri kuwa wakulima hao wanapata hela ndogo kwa sababu hakuna soko la uhakika na la moja kwa moja.

"Tuseme bei ziko chini maisha ya huyu mkulima bado siyo mazuri yapo ya wastani kwa maana kipato ni kidogo na ndiyo maana tunazidi kuwahimiza wasitegemee nanasi zaidi, wategemee na mazao mengine kama parachichi labda walime migomba, kulima maharage ili soko linapokuwa limeyumba wanaweza kupata na kitu kingine," anasema Mfugale.

Alisema katika jitihada za kutafuta soko waliongea na halmashauri ili kuwaletea kiwanda lakini wakaleta mtambo mdogo ambao haukuweza kukidhi mahitaji ya wakulima hao.



# Ujenzi wa makazi chanzo kupungua uzalishaji viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar imesema uzalishaji wa bidhaa za viungo umepungua kutokana na maeneo ambayo yalikuwa yanatumika kwa ajili ya kilimo kuwa makazi ya watu.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Omar Said Shaban katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir.

Ameir alitaka kujua ni mtarajio yapi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya viungo nchini ili kukidhi soko la kimataifa.

Alisema matarajio ya Serikali ni kuona kwamba Zanzibar inaendelea kusifika na kwa uzalishaji wa bidhaa za viungo vikiwemo uzile, mdalasini na vilina, kwamba Serikali itaendelea kuwahimiza wakulima kulima kwa wingi mazao hayo.

Waziri Shaban alisema pia wataendelea kuwapatia mafunzo na kuwatafutia masoko zaidi wakulima wa mazao hayo ili kunufaika na bei nzuri.

“Mheshimiwa Spika, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kupitia Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) imeendelea kuwajengea uwezo wakulima zaidi ya 100 juu ya uendelezaji wa mazao ya viungo, ambapo mafunzo hayo huwa yanafanyika kila mwaka na kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 yalifanyika Agosti, 2023” alisema.

Aidha alisema maeneo ya wakulima waliopatiwa mafunzo kwa upande wa Unguja ni Donge, Kizimbani, Matemwe na Makunduchi na Pemba ni Mkoani, Gando, Daya na Mtambwe.

Zanzibar inasifika duniani kwa uzalishaji wa viungo licha ya kwamba uzalishaji wa baadhi ya mazao hayo ukitoa zao la karafuu, haujakidhi mahitaji ya soko la kimataifa.



KATIBU wa Kamati Maalum ya NEC,Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUK) CCM Zanzibar, Khadija Salum Ali akizungumza na Balozi mdogo wa Msumbiji Zanzibar, Agostinho Abacar Trinza,mara baada ya kuwasili Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar kwa ajili ya mazungumzo ya kitaasisi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yazidi kujikita kidijitali, yazindua ZanVibali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Zena Ahmed Said amesema mfumo wa kutumia makaratasi katika kuomba vibali vya safari kwa watumishi umepitwa na wakati.

Amesema mfumo huo unatumia rasilimali nyingi zaidi kuliko mfumo wa kidijitali.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa watendaji wa serikali kuhusu mfumo wa vibali vya safari za nje ya nchi kwa njia ya kidigitali (ZanVibali).

Alisema mfumo huo utasaidia wafanyakazi wanapoomba vibali kuvipata kwa wakati bila ya usumbufu, lakini serikali itafaidika katika kupata taarifa muhimu.

“Mfumo huu wa ZanVibali utasaidia sana ili sasa wafanyakazi wanapoomba vibali vya safari nje ya nchi waweze kuvipata kwa wakati na bila ya usumbufu wowote, lakini kupitia mfumo huu serikali itafaidika kupata taarifa muhimu”alisema.

Alisema mfumo wa kutumia makaratasi inaugumu kupata taarifa zote hasa za watumishi kwa sababu kuna baadhi ya watumishi wanasafiri mara kwa mara, hivyo kupitia mfumo huo mpya vibali vya ruhusa alivyopewa vitajulikana pamoja na gharama zilizotumika.

Alisema kupitia mfumo huo pia serikali itaweza kuona wale watumishi wanaochelewa kutoa vibali vya safari kwa sababu zao zisizo na masingi.

Zena alisema serikali itaweza pia kujua kwa mwaka inatumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kuruhusu watumishi kwenda nje ya nchi.

“Baada ya mafunzo haya naamini mtaweza kupata ujuzi ambao utakuwezesheni kuutumia rasmi mfumo huu na kuondoa shida ambazo zilikuwa zikitupata za kutumia mfumo wa karatasi na naamini ikijitokeza changamoto wakala upo tayari kwa kutatua kwa haraka,” alisema.

Hivyo aliipongeza Serikali Mtandao kwa kuwapatia mfumo huo ambao utawezesha kuondoka katika kufanya kazi kwa kutumia makaratasi na kutumia rasilimali zaidi, hivyo kwenda kidijitali.

Alisema mfumo huo pia utamuwezesha mtumishi popote alipo kutumia simu yake ya kiganjani kufanya kazi na kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali ya Mtandao, Seif Said Seif, alisema lengo la mafunzo hayo ni kujenga uelewa watendaji hao kuhusu ZanVibali.

Alisema mfumo huo ni jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha huduma zote zinatolewa kupitia mifumo na kuweka serikali ya kidijitali.

“Jitihada zipo na zinaendelea lakini leo tumeona tuwaite watendaji wa taasisi ili waweze kufahamu jitihada za serikali na jitihada nyingine kuona tunashirikiana kwa pamoja katika kuleta mabadiliko ya kidijitali kwa Zanzibar na kuleta ufanisi zaidi na kutoa huduma kwa haraka,” alisema.

Aidha alisema E- Government ipo tayari kushirikiana na taasisi zote za serikali katika kuleta mabadiliko ambayo yataleta ufanisi zaidi katika kutoa huduma na kuileta Zanzibar ya kidijitali.

Katibu Mkuu wa wakala huo, Mansura Mosi Kassim, alisema hivi sasa serikali inakwenda katika utaratibu wa uombaji wa vibali kwa njia ya mtandao, ni moja ya mageuzi ya utendaji mzima wa serikali katika kutekeleza kazi zake.

Alisema ipo mifumo mbalimbali iliyoanzishwa na imeshaanza kutumika ikiwemo mfumo wa ZanMalipo, ZanAjira na E- Office ambayo ni moja ya jitihada za kuleta mageuzi katika utendaji kazi wa serikali ikiwemo kuongeza kasi na kupunguza urasimu, lakini pia kupunguza gharama za uendeshaji serikalini.

# Uimarishaji mifumo waipaisha ZRA ukusanyaji mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema uimarishaji wa mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi umeisaidia Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kuvuka malengo yake katika kipindi cha miezi sita.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Juma Makungu Juma katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe Ameir Abdulla Ameir.

Ameir alitaka kufahamu mikakati inayochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar katika ukusanyaji wa mapato na kuingiza fedha serikalini.

Akijibu swali hilo, Juma alitaja mikakati iliyochukuliwa ni pamoja na kubuni na kutengeneza mfumo wa utoaji wa risiti za kielektroniki, akisema mfumo huo umetengenezwa na wataalam wa ndani wa mamlaka kuanza kazi rasmi mwaka 2021.

Alisema mfumo huo unafanya kazi kwa kuwasajili walipa kodi wenye mauzo yasiyozidi Sh. milioni 10 kwa mwaka ambapo kwa mujibu wa sheria wanatakiwa kutumia mfumo huo.

Aidha alisema sheria imempa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kumtaka mfanyabiashara yoyote kutumia mashine hizo.

Alisema hadi kufikia Januari 2024 walipa kodi 8,161 wamesajiliwa kutumia mfumo huo na mashine 8,892 zimenunuliwa na wafanyabiashara.

Naibu waziri huyo alisema Mfumo wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Mapato (ZIDRAS) umeanza kufanya kazi kuanzia Julai 2023.

Alisema mfumo huo unatumika ikiwa ni mbadala wa mfumo wa zamani wa ZITAS ambao ulikuwa na changamoto na kushindwa kufanya kazi zake kikamilifu.

Juma alisema kuwepo kwa mifumo mipya ya ukusanyaji mapato kumeleta mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato, ambapo katika mwaka 2023-2024 makadirio ya makusanyo yalikuwa Sh.bilioni 401.9, makusanyo halisi yalikuwa Sh. bilioni 421.9 ikiwa sawa na ufanisi wa asilimia 104.9.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FRANCIS LONGIDU MOLLEL**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 785 AUB** Toyota Land Cruiser. Chasses Namba **HDJ810019320,** Engine Namba **IHD0038237.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **MOS/TR/RB/209/2024.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**IMANI BRAYSON KIDUNU**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 708 DEJ.** Chassis namba **MD6M14PA7M4L05118.** Engine namba **13102021A035.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **MKO/RB/23/2024.**

**The Land Disputes Courts (The District Land and Housing Tribunal)**
**Regulations GN.No.174/2003**
**Form No.2B**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**MAHALI: KIGOMA**
**MAOMBI NA...92...MWAKA...2023**
**ANGELA NKAYAMBA.........MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MAWAZO JUMA KALUKULA NA WENZAKE......MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**MAWAZO JUMA KALUKULA**
**BAHATI KAROLI**
**KITWANA MAULIDI**

Fahamu kwamba, shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe......6......Mwezi 03 Mwaka....2024 saa 2:30 Asubuhi/Mchana mbele ya Mheshimiwa M.Mwinyi Mwenyekiti wa Baraza, Hivyo unaamriwa kuhudhuria mnele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wanhu na Lakiri/Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 15...Mwezi ..02...Mwaka 2024.

CHAIRMAN DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL TANZANIA

MWENYEKITI

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEEP POLL**

BY THIS DEED POLL 1. The undersigned BENJAMIN LUKIO PALLANGYO a Tanzania citizen of ARUSHA Region formally known as BENJAMIN URASSA,BENJAMIN L. URASSA and BENJAMIN LUKIO URASSA , absolutely renounce and abandon the use said names of BENJAMIN URASSA, BENJAMIN L. URASSA,BENJAMIN LUKIO URASSA and in lieu thereof do assume the name of BENJAMIN LUKIO PALLANGYO.

IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid, I HEREBY DECLARE that, I BENJAMIN LUKIO PALLANGYO shall be known at all times thereafter in all records, deeds documents and other writing and instruments and in all actions and proceedings all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever, use and sign the said names of BENJAMIN LUKIO PALLANGYO as my name in lieu of my said former names of BENJAMIN URASSA, BENJAMIN L. URASSA,BENJAMIN LUKIO URASSA so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be called and known or distinguished not by my former names of BENJAMIN URASSA,BENJAMIN L. URASSA and BENJAMIN LUKIO URASSA but by my new name of BENJAMIN LUKIO PALLANGYO renounced as aforesaid.

IN WITNESS WHEREOF ,I have hereunder subscribed my adopted and substituted name of BENJAMIN LUKIO PALLANGYO .

SIGNED and DELIVERED at ARUSHA by The said BENJAMIN LUKIO PALLANGYO in my presence this 16th day of FEBRUARY, 2024 — DEPONENT

BEFORE ME

QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS



## KUPOTEA KWA CHETI



**MABULA SHIGALA RASHID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2869-0109** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MHANDU SEKONDARI mwaka 2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya polisi: PH/MWA/NYA/4142/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**MICHELLE MALLEO MREMA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 333 EAD – FORD RANGER.** Chassis namba **AFAPXXMJ2PLY40971.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 333 EAC – MERCEDES BENZ.** Chassis namba **WIK1771872J320843.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/3716/2024.**

## TANGAZO!

### MNADA WA HADHARA WA NG'OMBE

**FAGIO BROKERS** kwa amri ya **MAHAKAMA KUU KANDA YA MBEYA** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara Ng'ombe 92 waliopo **NOFA – INDUSTRIAL (MABATINI - MAGEREJINI).** Mnada utafanyika siku ya **IJUMAA tarehe 23/02/2024** kuanzia saa 3:00 kamili asubuhi.

**MASHARTI YA MNADA**

- Mshindi atalipa 100% ya bei ya Ng'ombe alionunua.
- Mnunuzi atatakiwa kuja na rangi kwa ajili ya kuweka alama ng'ombe alionunua.
- Mnunuzi atatakiwa kuja na usafiri/gari kwa ajili ya kusafirisha ng'ombe alionunua.

**MAWASILIANO**
**0786 606 041/0757 727 741**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/ PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**E-MAIL: advertise@guardian.co.tz**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
23.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 24-02-2024** hadi **27-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia **Mikumi**, gari hizo zina namba za usajili:

| | | |
|---|---|---|
| T 868DXS /T269DUH | T 781EAP/ T273DUH | |
| T295EDD/T630AJA | T807DYL/T877EAU | T998EDR/T272DUH |

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 24.00**
**Upana - mita 4.50**
**Kimo - mita 5.20**

2. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port,** hadi Kilombero kupitia **Pwani, Morogoro** hadi **Kilombero** gari zitasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Maandalizi ujenzi wa daraja Kavuu yaiva

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amekagua daraja la muda pamoja na maandalizi ya ujenzi wa daraja la Mirumba wilaya ya Mlele mkoani Katavi ambayo yamefikia hatua nzuri.

Daraja hilo linaunganisha mkoa wa Katavi na Rukwa lina urefu wa mita 60 na litagharimu Sh. bilioni 6.55.

Pinda alikagua daraja hilo jana ikiwa ni mwendelezo wa kukagua shughuli za maendeleo katika jimbo hilo sambamba na maandalizi ya mkutano mkuu wa jimbo hilo unaotarajiwa kufanyika kesho.

Akiwa katika eneo la daraja hilo, Pinda alioneshwa kuridhishwa na ujenzi wa daraja la muda pamoja na maandalizi ya lile la kudumu na kueleza kuwa daraja hilo litakuwa suluhisho ya shida ya muda mrefu ya wananchi wa Mirumba waliyokuwa wakiipata wakati wa mvua kubwa.

Mbunge huyo alisema anamwamini mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa daraja kutokana na kufanya kazi nzuri ya ujenzi wa daraja la Mwamapuli - Chamalendi alilosema lina kiwango bora na sasa limeanza kutumika.

''Mkandarasi, mimi sina tatizo na wewe na nina imani kazii hii ya ujenzi wa daraja la Mirumba itafanyika vizuri na kwa ufanisi. Nikutakie kila la kheri'' alisema Pinda.

Utekelezaji ujenzi wa daraja la Mirumba unafanywa na kampuni ya ujenzi ya Safari General Business Co Ltd JV Advance na ni wa miezi 24.

Katika hatua nyingine, mbunge huyo alitembelea vijiwe vya waendesha bodaboda kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Akiwa katika vijiwa hivyo, Pinda aliwataka waendesha bodaboda kuwa makini wakati wote wanapofanya kazi zao kwa kuwa umakini ndiyo utakaowawezesha kuepukana na ajali zinazoweza kuepukika.

Aidha, aliwaahidi waendesha bodaboda wa vijiwe vyote vya jimbo lake kuwapatia vizibao (Reflector) ili wavivae wakati wote wanapofanya kazi zao.

Waendesha bodaboda hao, mbali na kumshukuru mbunge kwa uamuzi wa kuwapatia 'reflector', walimwomba aangalie uwezekano wa kuwasaidia kupata mikopo ya pikipiki kutoka kwa kampuni zinazouza na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo.

# Sekta binafsi kushirikishwa uwekezaji wa Bagamoyo SEZ

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaishirikisha kwa karibu sekta binafsi katika kutekeleza mradi wa Kanda Maalumu ya Kiuchumi ya Bagamoyo (SEZ).

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilipotembelea Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji na Mauzo Nje ya Nchi (EPZA).

"Kuishirikisha kwa karibu sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi kama huu wa Bagamoyo ndio mwelekeo wa serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa mradi husika," alisema.

Mradi wa Bagamoyo SEZ ambao ulikuwa umesimama kwa zaidi ya miaka 10, umepata uhai tena baada ya hatua madhubuti iliyochukuliwa na Raisi Samia Suluhu Hassan ya kutaka uanze tena utekelezaji wake. Alisema ili kupata eneo la kutoka kutekeleza mradi wa Bagamoyo SEZ, serikali italipa fidia maeneo yote ambayo yanamilikiwa na wananchi kwa hatua.

Waziri Mkumbo alisema changamoto zinatokea ardhi ya wananchi anapochukuliwa lakini ulipaji wa fidia unashindikana, hivyo kuwafanya wananchi kuchukua maeneo yao.

Alisema tayari serikali inajenga miundombinu katika mradi wa Bagamoyo SEZ ikijuisha barabara, maji, mfumo wa maji taka, umeme na mfumo wa gesi asilia.

"Hii ndiyo namna bora zaidi ya kuandaa maeneo ya uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji makini kutoka sehemu mbalimbali duniani," alisema.

Alisema duniani kuna wawekezaji wengi sana lakini ili kupata wawekezaji makini inahitaji kuweka mazingira ya Uwekezaji kuwa mazuri ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu.

Prof. Mkumbo alisema katika utekelezaji wa mradi wa Bagamoyo SEZ, wawekezaji wanaweza kuungana wawili au watatu ili kuweka urahisi wa upatikanaji wa fedha za mradi.

Alisema hivi karibuni, walitembelea Benin ambako wanatekeleza mradi kama huo wa na kuona kwamba wamefuata mfumo wa ushirikiano na sekta binafsi ambapo serikali ina hisa asilimia 50 na sekta binafsi asilimia 50.

Mwaka jana serikali ilisema ili kutekeleza mradi huo, Sh. trilioni 11 zinahitajika na kati ya fedhas hizo, serikali itatoa Sh. trilioni 1.6 kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya msingi kama barabara, umeme, maji na mfumo wa majitaka.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Selemani Zedi, aliahidi kutoa ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa Bagamoyo SEZ kutokana na umuhimu wake katika uchumi wa nchi.

"Napenda kuwaahidi kuwa kamati yangu itatoa ushirikiano wa Karibu sana ili kuhakikisha kuwa mradi huu unakuwa na Mafanikio makubwa sana ili uweze kuchangia Uchumi wa nchi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, alisema Bagamoyo SEZ itajengwa miundombinu mbalimbali ikiwamo umeme, maji,mfumo wa maji taka na gesi asilia.

Pia alisema kuwa asilimia 43 ya eneo la utekelezaji wa mradi huu ambalo ni hekta 8,676 limeshalipwa fidia na maeneo mengine yanafanyiwa utaratibu mpya wa kuwashirikisha na kuyaingiza maeneo ya watu kuwa sehemu ya mradi huu.

Mradi huo utakuwa na manufaa makubwa katika uchumi wa taifa, ukuaji wa tekinolojia na kutoa ajira hasa kwa vijana.



Sehemu ya washiriki wa mafunzo kwa watendaji wa Uchaguzi mdogo wa udiwani kwa Kata 23 za Tanzania bara yaliyofanyika mkoani Morogoro kwa siku tatu. Uchaguzi unatarajiwa kufanyika Machi 20,2024. **PICHA: NEC**

# Wasimamizi uchaguzi wahimizwa ufanisi

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imewakumbusha watendaji katika uchaguzi mdogo wa kata 23 za Tanzania Bara, kukamilisha maandalizi muhimu kwa wakati ili kuwezesha kufanyika kwa ufanisi.

Wito huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Jaji Mstaafu Mbarouk Salim Mbarouk, wakati akifunga mafunzo kwa watendaji hao yaliyofanyika mkoani hapa.

Uchaguzi huo utafanyika Machi 20, mwaka huu na fomu za uteuzi zitatolewa kuanzia Februari 27 hadi Machi 4 na uteuzi wa wagombea Machi 4 huku kampeni za uchaguzi zikitarajiwa kufanyika kuanzia Machi 5 hadi 19.

"Mnatakiwa kukamilisha mambo yote muhimu yanayotakiwa kwenye mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na kubandika matangazo na mabango mbalimbali ya kisheria kuhusiana na uchaguzi kwa mujibu wa maelekezo," alisema.

Jaji Mbarouk aliwakumbusha watendaji hao kuwa kuna wadau mbalimbali wa uchaguzi kama vile vyama vya siasa, wananchi na watazamaji ambao wanafuatilia uendeshwaji wa uchaguzi na kiwango cha uzingatiwaji wa sheria zinazohusiana na uchaguzi, hivyo ni muhimu wakatekeleza kila hatua na kila jambo linalotakiwa kwa mujibu wa kalenda ya uchaguzi.

"Jukumu lililoko mbele yetu ni kubwa na muhimu na linahitaji umakini na kujitoa hasa baada ya kupatiwa mafunzo haya, mtatekeleza majukumu yenu kwa ufanisi na weledi mkizingatia ratiba ya utekelezaji ili kufanikisha uchaguzi wa Machi 4," alisema.

Makamu mwenyekiti alisisitiza umuhimu wa watendaji hao kutenga sehemu ya muda wao kusoma Katiba, sheria na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Tume ili yawaongoze katika kusimamia uchaguzi utakaokuwa huru na wa haki.

Kata zitakazofanya uchaguzi huo mdogo na halmashauri kwenye mabano ni Kimbiji (Kigamboni), Kasingirima (Kigoma/Ujiji), Ndevelwa (Manispaa Tabora), Msangani (Mji Kibaha), Fukayosi (Bagamoyo), Mlanzi (Kibiti), Utiri (Mji Mbinga) na Mbingamhalule (wilaya ya Songea).

Zingine ni Isebya (Mbogwe), Kibata (Kilwa), Mshikamano (Musoma), Busegwe (Butiama), Nkokwa (Kyela), Kamwene (Mlimba), Chipuputa (Nanyumbu), Buzilasoga (Sengerema), Mhande (Kwimba), Kabwe (Nkasi), Bukundi (Meatu) Mkuzi (Muheza) na Boma, Mtimbwani na Mayomboni zote Mkinga.

# PRISONS YATAMBA KUIPA KICHAPO AZAM JUMAPILI

**Oliver Albert na Shufaa Lyimo**

MAAFANDE wa Tanzania Prisons wametamba wako tayari kuikabili Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya lakini hawataingia 'kichwa kichwa' kwa sababu wanajua wapinzani wao wako 'moto' kwa sasa.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Mtupa, alisema wanaendelea vyema na maandalizi ya kuiwinda Azam wakitarajia mchezo huo utakuwa mzuri na mgumu.

Mtupa alisema Azam wamefanya usajili mzuri msimu huu na ni moja ya timu yenye mbinu 'kali' uwanjani hivyo lazima wajipange vizuri kuwakabili.

"Tunajua tunacheza na timu kubwa ambayo iko moto kwa sasa na yenye wachezaji wenye uwezo mkubwa, hivyo tunaendelea kujipanga. Tunaendelea kufanyia kazi baadhi ya vitu kwenye uwanja wa mazoezi ili siku ya mechi tuwe vizuri na kupata matokeo, malengo yetu msimu huu ni kumaliza ndani ya nafasi nne za juu sasa ili uzipate nafasi hizo lazima ujitoe hasa, "alisema Mtupa.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hamad Ally, amesema wanaendelea kufanyia kazi mapungufu katika safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha Jumapili wanapata mabao na wanazibakisha pointi tatu nyumbani.

**"Marekebisho ninayoendelea kuyafanya naamini yatanipa matokeo mazuri katika mchezo huo ambao utakuwa na upinzani mkubwa, " alisema Ally.**

Kocha huyo alisema lengo lake ni kushinda michezo yote ya nyumbani ikiwa pamoja na kushika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema wachezaji wote wanaendelea vyema kiafya na kudai kwa wale ambao walikuwa majeruhi hali zao zinaendelea kuimarika.

Aliongeza nyota wake, Salum Kimenya na Doto Shabani, ambao walikuwa wamepata majeraha kwa sasa wameanza kufanya mazoezi mepesi mepesi.

Prisons katika mechi tano zilizopita imeshinda tatu, imetoka sare mechi moja na kupoteza mchezo moja dhidi ya Yanga wakati Azam katika mechi zake tano zilizopita imeshinda tatu na kutoka sare mechi mbili.



Miss Tanzania 2022, Halipa Kopwe, akipeperusha bendera ya Taifa muda mchache kabla ya kuelekea India kushiriki mashindano ya urembo ya dunia (Miss World 2024), yatakayofanyika Machi 9, mwaka huu katika mji wa Mumbai nchini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waogeleaji 217 kuchuana Dar

**Na Shufaa Lyimo**

WAOGELEAJI 217 kutoka klabu mbali mbali za nje na ndani ya Tanzania wanatarajia kuchuana katika mashindano ya Tallis-IST yatakayofanyika kuanzia kesho kwenye Bwawa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika iliyopo Masaki, Dar es Salaam. Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa klabu ya Tallis-IST, Khadija Shebe, alisema mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji vijana wenye umri tofauti tofauti.

Shebe alisema waogeleaji hao wametoka katika klabu 17 za ndani na nje ya nchi ambazo zimethibitisha kushiriki mashindano hayo.

Alitaja nchi ambazo zitaleta washiriki ni pamoja na Kenya, Uganda, Zanzibar na wenyeji Tanzania.

"Mashindano haya ni makubwa na hufanyika kila mwaka, mwaka huu yamefanyiwa maboresho makubwa kuhakikisha kila nchi inafanya vizuri," alisema Shebe.

Meneja huyo alisema maandalizi yanaendelea vyema na anawashukuru wadhamini pamoja na taasisi mbalimbali ambazo zimewaunga mkono kwa sababu mashindano hayo yatasaidia kuutangaza mchezo huo ambao kwa sasa unazidi kukua.

## Dar City, JKT mechi ya kisasi na rekodi

**Na Oliver Albert**

NI kama fainali inajirudia tena, unaweza kusema hivyo baada ya ratiba ya Ligi ya Kikapu Mkoa wa Dar es Salaam (BDL) kutoka ambapo mabingwa watetezi, Dar City watafungua pazia kwa kucheza dhidi ya JKT mchezo utakaofanyika Machi 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Don Bosco, Upanga.

Timu hizo ndizo zilikutana fainali ya ligi hiyo mwaka jana na Dar City kushinda mechi ya mwisho kwa pointi 69-63 na kutwaa ubingwa.

Ushindi wa mechi tatu kati ya nne za fainali ndizo ziliamua ubingwa wa Dar City, ambayo ilishinda mechi tatu kwa pointi 75-61, 75-56 na 69-63 wakati JKT walishinda mechi moja tu kwa pointi 68-55.

Sasa fainali hiyo inarejea tena katika mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo msimu huu na swali je JKT watalipa kisasi au Dar City wataendelea kuwa wababe?.

Kocha wa JKT, Christian Jacob 'Webber' alisema wanajipanga kufanya vizuri katika mechi ya ufunguzi.

"Itakuwa mechi ngumu kwa sababu Dar City tulikutana nao fainali na wakatufunga, tukakosa ubingwa, ila safari hii mechi hiyo lazima tulipe kisasi, hatutakubali kufungwa mara mbili, " alisema Jacob.

Kocha Mkuu wa Dar City, Mohammed Mbwana, alisema wako tayari kuanza ligi hiyo vizuri ili kutetea ubingwa wao.

"Unapoanza ligi kwa ushindi ndio morali inakuwa juu zaidi, tunajua itakuwa mechi ngumu, najua wapinzaji wetu watakuja kwa nguvu zaidi kwa sababu tuliwafunga katika fainali msimu uliopita hivyo lazima watataka kulipa kisasi, lakini hata sisi tuko vizuri, acha ligi ianze, "alisema Mbwana.

Mechi nyingine za ufunguzi ligi hiyo kwa wanaume itakuwa kati ya DB Oratory dhidi ya Srelio wakati kwa wanawake kutakuwa na mechi tatu, Jeshi Stars itakayocheza dhidi ya 'ndugu zao' Twalipo Queens huku Mgulani Stars itaikabili JKT Stars wakati mabingwa watetezi kwa wanawake, Vijana Queens wataonyeshana kazi na City Queens.

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inaongoza mbele ya Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25 msimu unaokuja. (***TeamTalks***)

### SOLANKE KUTUA BOURNEMOUTH

KLABU ya West Ham inatazamia kumnunua mshambuliaji wa Bournemouth mwenye umri wa miaka 26, Dominic Solanke. (***Telegraph***)

### TUCHEL KUREJEA ENGLAND

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel ataweka kipaumbele cha kurejea England atakapoondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani mwishoni mwa msimu huu. (***Telegraph***)

### KLOPP AIKATAA BAYERN

JURGEN Klopp hatachukua nafasi ya Thomas Tuchel katika klabu ya Bayern Munich mara baada ya kuondoka Anfield mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa wakala wa kocha huyo wa Liverpool. (***Sky Sports Germany***)

### GIROUD ANUKIA MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa AC Milan na Ufaransa, Olivier Giroud, mwenye umri wa miaka 37 anaweza kuondoka katika klabu hiyo na kwenda Ligi Kuu ya Soka ya Marekani (MLS), mwishoni mwa msimu huu. (Corriere dello Sport – Via Itali)

### SANCHEZ AINGIA SOKONI

CHELSEA itasikiliza ofa kwa mlinda mlango wa Hispania, Robert Sanchez, msimu huu wa joto na The Blues wanaweza kumnasa ili kuchukua nafasi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Football Insider***)

### CHELSEA KUTOMUUZA COLWILL

CHELSEA haitasikiliza ofa kwa mlinzi wa England, Levi Colwill, mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa na Paris St-Germain pamoja na Liverpool. (***Standard***)

### MODRIK KUONDOKA MADRID

KIUNGO wa kati wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Croatia, Luka Modric, anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto. (***Bild***)

### SALAH, SON WATAJWA SAUDIA

KLABU ya Al-Ittihad itamlenga mshambuliaji wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 31, Son Heung-min na mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah katika dirisha la usajili la majira ya joto. (***Football Transfers***)


### UNITED, ARSENAL VITANI

KLABU ya Manchester United na Arsenal zinamtaka mshambuliaji wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 18, Mathys Tel, ambaye ni raia wa Ufaransa. (***Bild – In Germany***)

### SPURS YAMTAKA GARNER

KIUNGO wa kati wa Everton, James Garner, analengwa na Tottenham Hotspur na Newcastle United, huku raia huyo wa England mwenye umri wa miaka 22 akivutia pande nyingi za Ligi Kuu England. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AWAKARIPIA WACHEZAJI ARSENAL

**LISBON,** Ureno

### ●●● Kocha huyo hakuridhishwa na kiwango huku wakilala 1-0...

MIKEL Arteta aliwabwatukia wachezaji wa Arsenal kwa kukosa "tishio langoni" wakati walipokubali kichapo cha 1-0 kutoka kwa Porto katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Mbrazil Galeno alifunga bao la dakika za lala salama na kuwapa wenyeji faida kuelekea mchezo wa marudiano utakaochezwa Machi 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Emirates.**

Ulikuwa mchezo usiovutia kutoka kwa Arsenal na Arteta mwenye umri wa miaka 41, hakujizuia katika tathmini yake kwa uchezaji.

Aliiambia TNT Sport: "Tulikosa tishio. Tulikosa uvamizi, haswa na mpira katika nafasi ya tatu ya mwisho. Tunaweza kufanya vizuri zaidi.

"Tunapaswa kusimamia vyema zaidi. Hatuwezi kushinda kwa jinsi tulivyoudhibiti mpira mara tatu kwenye maeneo ya kina.

"Ikiwa unataka kutinga hatua ya robo fainali lazima umshinde mpinzani wako na hii ndio tutalazimika kufanya kule Emirates sasa."

Porto wangeweza kufunga mapema kabla ya bao lao la dakika za mwisho, wakati Galeno alipokosa nafasi nzuri ya kufunga dakika ya 21.

Arteta aliisifia timu hiyo ya Ureno, ambayo ilijilinda vyema kwa muda mrefu.

Mhispania huyo aliongeza: "Nadhani ni timu ambayo imejipanga vyema katika kujilinda.

"Kuna mambo fulani ambayo tutalazimika kufanya vizuri zaidi, tunajua nini cha kutarajia."

Declan Rice, aliyeshiriki katika mchezo wake wa kwanza wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na alielezea jinsi timu yake ushindi.

Alisema: "Ikiwa 0-0, unatazama saa na dakika 93 zimekwisha, ikiwa hautashinda mchezo basi usipoteze.

"Labda tuwe na ufahamu kidogo kuhusu sisi kusalia na kupata sare katika uwanja mgumu dhidi ya mpinzani mgumu. Mengi ya kuchezea katika mkondo wa pili."

# VAN DIJK: TUPO KATIKA NJIA SAHIHI




**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk aliwapongeza Liverpool baada ya kutoka nyuma na kuwashinda Luton 4-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa kwenye Uwanja wa Anfield, juzi.

Wekundu hao walikuwa wamekwenda mapumziko wakiwa nyuma ya Luton walio hatarini kushuka daraja kupitia kwa bao la kichwa lililofungwa na Cheidozie Ogbene.

Lakini mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Van Dijk, Cody Gakpo, Luis Diaz na Harvey Elliott yalipata ushindi mnono na kurejesha uongozi wao wa pointi nne kileleni katka Ligi Kuu England.

Nahodha huyo wa Liverpool mwenye umri wa miaka 32, ambaye alianza kurejea kwa bao lake la kichwa dakika ya 56, alisema: "Hakuna aliyeridhika na kipindi cha kwanza. Tulikuwa tukikimbilia katika nafasi ya tatu ya mwisho na hatukupata pasi sahihi.

"Ni wazi ni kawaida kuwa na wasiwasi mbele wakati haufanyi maamuzi sahihi. Mwitikio ulioonyeshwa leo (juzi) ulikuwa mzuri na kitu tunachohitaji kwa msimu mzima leo (juzi) ulikuwa mkubwa.

"Luton ni timu nzuri na wanacheza mpira wakichukua hatari na tuliposhinda mpira ilibidi tuwaadhibu."

Beki huyo wa kati wa Uholanzi aliongeza: "Ni muhimu kwetu kuangalia mbele ni nani tunayekutana naye, lakini leo (juzi) ilikuwa muhimu na ngumu kwa sababu nyingi.

"Sidhani kama kulikuwa na majeraha yoyote kutoka usiku wa leo (juzi) na sasa ni wakati wa kuzingatia fainali."

# Barcelona ilikosa ukomavu - Xavi

**NAPLES,** Italia

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernández, alihisi timu yake haikukomaa wakati mabingwa hao wa Hispania walipolazimishwa sare ya 1-1 dhidi ya Napoli kwenye Uwanja wa Maradona katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa juzi.



Robert Lewandowski aliifungia Barca bao la kuongoza, lakini bao la kusawazisha la Victor Osimhen dakika ya 75 kwa mabingwa hao wa Italia lilihakikisha timu hizo zitaingia katika mchezo wa mkondo wa pili Machi 2, mwaka huu zikiwa sare.

"Ni hisia chungu kwa sababu tulikuwa na mchezo mikononi mwetu," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tulicheza vizuri. Tulijilinda vyema, lakini baada ya kuchukua uongozi tulikosa udhibiti tulipohitaji kutawala, kuonyesha utu na kuwa wakali.

"Ni aibu. Ilikuwa utendaji mzuri kwa ujumla na ninajivunia picha ambayo tumeonyesha Ulaya. Hii ndiyo Barca tunayoitaka, lakini tulikosa ukomavu wa kusimamia mchezo.

"Labda kimwili walikuwa na nguvu kuliko sisi katika pambano la watu binafsi, lakini tukicheza hivi tuna nafasi nzuri ya kuvuka na tutashinda zaidi ya tunavyopoteza."

Katika mchezo wa kwanza wa mtoano wa Ligi ya Mabingwa kwa Barca tangu 2021, Lewandowski aliendeleza kasi yake nzuri na kufungua ukurasa wa mabao katika kipindi cha pili, akimalizia vyema baada ya kupokea mpira kutoka kwa Pedri.

Mshambuliaji huyo wa Poland sasa amefunga mabao matano katika michezo yake minne iliyopita katika michuano yote, na kufikisha jumla ya mabao 18 kwa msimu huu baada ya kuifungia Barca bao lake lake la 50 wikendi iliyopita.

"Lewandowski anachezea kitimu sasa," aliongeza Xavi. "Amepiga hatua mbele. Anashinda vita vyake binafsi, yuko pamoja na timu na anapiga hatua kubwa.

"Yeye ni kiongozi wa asili na anataka kuimarika. Anasaidia sana kwa sasa na ni zaidi kuhusu hilo, mabao ni matokeo ya uchezaji wake mzuri."

Barca, ambao wako pointi nane nyuma ya vinara wa LaLiga, Real Madrid, wana mechi za ligi dhidi ya Getafe, Athletic Club na Mallorca kabla ya mchezo wa marudiano dhidi ya Napoli hapo Machi 12, mwaka huu.

Mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Olympic huku kazi ya kuijenga upya Camp Nou ikiendelea.

"Bila shaka tunaikosa Camp Nou," alisema Xavi, ambaye atajiuzulu mwishoni mwa kampeni, akizungumzia kuhusu kulazimika kucheza nje ya uwanja wa nyumbani wa klabu hiyo unaobeba mashabiki 100,000.

"Nilisema kabla ya msimu ujao utakuwa mwaka mgumu mbali na uwanja.

"Sio sawa kucheza Uwanja wa Olimpiki kama Camp Nou, lakini haipaswi kutuathiri. Ni aibu kwa sababu fikiria mechi ya mkondo wa pili Camp Nou, itakuwa tofauti, kwetu na kwa wapinzani."

# Tuchel kuondoka Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, ataondoka mwishoni mwa msimu huu, klabu hiyo ilitangaza juzi.

Mustakabali wa Tuchel ulikuwa chini ya uvumi unaoendelea huku klabu hiyo ikiachwa pointi nane na vinara wa Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, Bayer Leverkusen.

Bayern Munich wamepoteza michezo yao mitatu iliyopita, mechi mbili za Bundesliga mikononi mwa Leverkusen na Bochum, na pia kipigo cha 1-0 kutoka kwa Lazio katika mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Bayern Munich kupoteza mechi tatu za mashindano mfululizo tangu Mei, mwaka 2015, wakati tayari walikuwa wameshinda taji la Bundesliga.

"Tumekubaliana tutamaliza uhusiano wetu wa kikazi mwishoni mwa msimu huu. Hadi wakati huo, bila shaka nitaendelea kufanya kila niwezalo na wasaidizi wangu ili kupata mafanikio ya hali ya juu," alisema Tuchel katika taarifa yake.


Iwapo Bayern Munich watashindwa kuipiku Leverkusen, itakuwa ni mara ya kwanza tangu msimu wa 2011-12 kumaliza msimu bila taji la nyumbani.

Tuchel alichukua nafasi ya Julian Nagelsmann Machi, mwaka jana wakati klabu hiyo ikiwa pointi moja tu kileleni mwa Bundesliga na ingali kwenye Ligi ya Mabingwa.

Aliwaongoza kutwaa taji la ligi msimu uliopita, lakini akafanikiwa kutwaa taji hilo siku ya mwisho baada ya kushindwa kwa Borussia Dortmund kuifunga Mainz.

Majira ya joto ya yalishuhudia Bayern Munich wakimsajili Harry Kane kutoka Tottenham Hotspur kwa mkataba wa thamani ya euro milioni 120 na Kim Min-Jae kutoka Napoli kwa euro milioni 50.

Lakini dirisha hilo pia lilishuhudia Lucas Hernández, Ryan Gravenberch, Benjamin Pavard na Sadio Mané wote wakiondoka.



## Yanga SC yawabadilishia 'dawa' CR Belouizdad

INATOKA UK 24

hamu wapinzani wao pia wanakuja kwa ajili ya kusaka ushindi wa ugenini, wanafahamu ubora wa safu ya ulinzi na ushambuliaji ya CR Belouizdad, hivyo wamejipanga 'kuwamaliza' hapa nyumbani.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na leo (jana) jioni walifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao watautumia katika mechi hiyo ya kimataifa.

Kamwe alisema wanaendelea na hamasa kwa ajili ya kuhakikisha mashabiki wanajitokeza kwa wingi uwanjani ili kushuhudia timu yao inavyopambana kusaka ushindi na kuifanya safari ya kutafuta tiketi ya robo fainali ikamilike.

Naye Kocha Mkuu wa CR Belouizdad, Marcos Paquette, alisema wamejiandaa vizuri na wamekuja kutafuta matokeo chanya na aliweka wazi kundi lao halina ugumu kwa sababu kila timu inapambana kutafuta pointi tatu.

"Tumekuja kutafuta ushindi, tunatambua ugumu wa mchezo huu, tumetoka kucheza mechi hivi karibuni na sasa tupo tayari kuvaana na Yanga," alisema Marcos.

## *Simba SC: Tutawafurahisha*

INATOKA UK 24

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Pyramid FC iko tayari kumtoa kwa mkopo mshambuliaji huyo wa zamani wa Yanga baada ya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi chake.

Chanzo chetu kinasema mbali na Simba, Azam FC pia ya Tanzania inatajwa kuwasilisha ofa ya kumnasa Mkongomani huyo ambaye alikuwa na msimu mzuri na Yanga.

"Inaelezwa viongozi wameshapeleka barua ya ofa kwa Waarabu (Pyramid) kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji huyo kwa ajili ya msimu ujao ili kuimarisha safu ya ushambuliaji.

Uamuzi huo umefuatia mapungufu ya safu hiyo katika kikosi chetu, bado haijatulia licha ya kuongeza watu wawili katika usajili wa dirisha dogo, tunahitaji kuboresha tena kwa kupambana kupata huduma ya mtu kama Mayele," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza mbali na Mayele, pia wapo wachezaji ambao majina yao yameshawasilisha na skauti wanaofanya kazi kutokana na mapendekezo ya ripoti ya benchi la ufundi.

"Hatuna presha juu ya uwezo wake kwa sababu aliwahi kucheza hapa, kila mmoja anafahamu ubora wa Mayele, hivyo hatuna hofu juu ya ofa hiyo kwa sababu tutahitaji kuboresha kikosi chetu katika kila eneo ambalo linaonekana lina mapungufu," aliongeza mtoa habari wetu.

# TWIGA STARS, AFRIKA KUSINI MACHO PARIS

**Na Saada Akida**

HUKU ikimkosa straika wake nyota, Aisha Masaka, kutokana na kuwa majeruhi, Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuikaribisha Afrika Kusini (Banyana Banyana), katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Michezo ya Olimpiki imepangwa kufanyika kuanzia Julai 26 hadi Agosti 11, mwaka huu katika jiji la Paris, Ufaransa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, alisema kwa asilimia kubwa maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na wanasubiri muda tu ufike.

Shime alisema mechi hiyo ni kubwa kwa kila mchezaji anajipanga kuweka historia kwa mara nyingine.

"Nawapongeza wachezaji wangu kupambana hadi kufikia hatua hii ya mwisho kutafuta nafasi ya kufuzu Olimpiki, tunaenda kucheza mchezo mkubwa kulingana na wapinzani tunaokutana nao.

Tukumbuke tunacheza na mabingwa wa Afrika, hatuwezi kuwa wakubwa hadi tucheze na timu kubwa, tunahitaji kucheza Olimpiki hivyo hatuwezi kukwepa kukutana na timu kubwa kama Afrika Kusini na Algeria," alisema Shime.

Aliongeza Watanzania wanatakia kuendelea kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwapa nguvu wachezaji wao kwa sababu wanaiwakilisha Tanzania na si Twiga Stars pekee.

Nahodha wa Twiga Stars, Oppa Clement, alisema mchezo wa leo ni mkubwa kutokana na kukutana na timu kubwa ya Afrika ambapo kila mchezaji yuko tayari kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo mazuri.

Oppa alisema hawana presha yoyote kuelekea mchezo huo kwa sababu wamepewa maelekezo ya kusaka ushindi kwa ajili ya kusonga mbele katika michuano hiii.

Kocha Mkuu wa Banyana Banyana, Desiree Ellis, alisema maandalizi ya timu yake yako vizuri na wote wanafahamu huo ni mchezo muhimu na wamekuja kusaka ushindi dhidi ya Tanzania.

"Tumefanya maandalizi na tupo tayari kutafuta matokeo mazuri, tunafahamu hautakuwa mchezo rahisi lakini tumekuja kutafuta matokeo chanya," alisema Desiree.




Rais wa Yanga, Hersi Said (kushoto), akipongezana na mwakilishi wa Kampuni ya Karimjee Mobility, baada ya kusaini mkataba wa udhamini wenye thamani ya Sh. milioni 300 na utadumu kwa muda wa miezi 18. **PICHA: MTANDAO**

# Njia zitakazofungwa Kili Marathon 2024 zatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

ZIKIWA zimebakia siku chache kabla ya kufanyika mbio maarufu za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon kwa mwaka wa 2024, waandaaji wa mbio hizo wametoa maelezo kuhusu baadhi ya barabara zitakazofungwa keshokutwa katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, imeelezwa.

Kwa mujibu wa waandaaji hao, Barabara ya Sokoine kutoka kona ya KCMC hadi Kilimanjaro zitafungwa kuanzia saa 12 :00 hadi saa 3:30 asubuhi, ambapo wenye magari wanashauriwa kutumia njia ya eneo la Shanty Town na Kata ya Rau hadi eneo la Mweka, Kibosho.

Pia Barabara ya Kilimanjaro hadi kona ya Barabara ya Sokoine inayoelekea hospitali ya Rufaa ya KCMC itafungwa kuanzia saa 1:45 hadi saa 3:30 asubuhi.

"Hatua hii itatoa fursa washiriki wanaofika eneo la kuanzia mbio hizi kupata maeneo ya maegesho katika viwanja vya Shule ya Polisi Tanzania (CCP) pamoja na eneo la lango kuu la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kuelekea Uru sambamba na kupata nafasi ya kutosha kwa washiriki wakati wa kuanza kwa mbio hizo", ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya waandaaji, barabara ya Masoka hadi Mweka kupitia eneo la Kibosho pia kuanzia saa 12:30 hadi saa 2:30 asubuhi.

"Kutakuwa na maegesho ya bure kwenye eneo la CCP, ambapo wanaotaka kuegesha vyombo vyao vya moto wataingilia kupitia Barabara ya Kilimanjaro na eneo ambalo mbio za nusu marathon za Tigo (Tigo Half Marathon) zitaanzia.

Pia kutakuwa na maegesho ya bure kwenye eneo lenye kivuli kizuri katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) amalo linaweza kufikiwa kwa kupitia barabara inayoelekea Uru tu; ene hilo ni mwendo wa dakika tano tu kutoka uwanjani hadi eneo ambalo mbio za kilomita tano na zile za kilomita 21 zitaanzia na dakika mbili kutoka pale za kilomita 42 zitaanzia.

Wakati huo huo, zoezi la ukusanyaji wa namba na vifaa kwa ajili ya ushiriki wa mbio hizo mwaka huu ulianza jana na utamalizika kesho kwenye Uwanja wa Ushirika.

Mgeni rasmi katika mbio hizi za Jumapili ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Dk. Damas Ndumbaro.

# Michezo

Nipashe

Ijumaa Februari 23, 2024




Arteta awakaripia wachezaji Arsenal UK. 21



## Yanga yawabadilishia 'dawa' CR Belouizdad

**Na Saada Akida**

IKIWA na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amekiri ana kibarua cha kuimarisha kikosi chake kutokana na ugumu wa mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad kutoka Algeria utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema anafahamu vyema mchezo huo hautakuwa rahisi kutokana na kundi lao lilivyo na watashuka uwanjani huku kila timu ikihitaji pointi zitakazowaimarisha katika msimamo.

Gamondi alisema amewaandaa wachezaji wake kusaka ushindi na kuhakikisha CR Belouizdad hawafanyi mashambulizi ambayo yanaweza kuwapatia ushindi.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanafanikiwa kupata ushindi katika mchezo huo kwa sababu ameshapata mwelekeo mzuri katika mifumo yake ikiwemo kuanzisha mashambulizi kwa kutumia mawinga pamoja na viungo.

"Maandalizi yetu yanaendelea vizuri, tumefanikiwa kusahihisha makosa yetu na tunatambua utakuwa mchezo mgumu ukizingatia tunahitaji ushindi, tunachokitafuta kwa sasa ni pointi tatu, baadaye ndio tuanze kufikiria idadi ya mabao mengi," alisema Gamondi.

Aliongeza wanawafa-

INAENDELEA UK 23



Zimbwe Jr'

# Simba: Tutawafurahisha

## ●●● Yaanza mchakato wa kumnasa kwa mkopo Mayele katika usajili...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Simba inatarajia kuwavaa wenyeji Asec Mimosas katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku kwenye Uwanja wa Felix Houphouet Boigny jijini Abidjan, Ivory Coast, straika wa Pyramid FC, Fiston Mayele, anatajwa kutua kwa mkopo kwa Wekundu wa Msimbazi.

**Asec Mimosas yenye pointi 10 ndio vinara wa Kundi B wakifuatiwa na Simba yenye pointi tano, Jwaneng Galaxy ikishika nafasi ya tatu na pointi zake nne wakati Wydad Casablanca inaburuza mkia ikiwa na pointi tatu.**

Simba itaingia katika mechi hiyo ikiwa na kazi moja ya kusaka ushindi ili kuimarisha matumaini ya kusonga mbele katika michuano hiyo huku wapinzani wao tayari wameshafuzu hatua inayofuata.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema timu yao ina matumaini ya kuibuka na ushindi kwa sababu wachezaji wote wanajua umuhimu wa mechi hiyo, wakifanya vikao vya kujipanga na kuhamasishana.

"Matumaini naona ni makubwa ya kupata ushindi kwa sababu hata wachezaji wanajua umuhimu wa mechi hii, hata wao kwa wao wanakaa na kuongea wanahamasishana kuwa ushindi katika mechi hii watakuwa tayari wameingiza mguu mmoja kwenda robo fainali, kwa kulitambua hili inatupa matumaini sisi kama benchi la ufundi kuwa tunakwenda kufanya vizuri katika mchezo huu," alisema Matola.



Kocha huyo alisema kuna wepesi ambao wanauona baada ya kubaini kikosi cha wapinzani wao kimekaa muda mrefu bila kucheza mechi, lakini pia kuna ugumu wa aina fulani kwa sababu watakutana nao wakiwa hawana cha kupoteza.

"Tunakwenda kucheza na timu ambayo haijacheza hata mchezo mmoja tangu mapumziko ya AFCON, hawana mechi yoyote katika miezi hii miwili na sisi tumecheza mechi kadhaa ya Ligi Kuu na Kombe la FA, hii inaweza kuwa na faida kubwa kwetu, ni jinsi gani tu ya kujipanga na kutumia madhaifu hayo.

Sababu nyingine watajiona wameshapita na wanaweza kudharau mechi, wakawa wanajiandaa na hatua ya robo fainali, wakauchukulia poa na wanaweza hata kubadili kikosi na kuwapumzisha wachezaji wao tegemeo," Matola alisema.

Aliongeza ugumu walionao ni kujipanga kutibua rekodi ya kutopoteza mechi yoyote mpaka sasa, pia kutaka kumaliza wa kwanza katika kundi kwa sababu wakifanya hivyo watakwenda kucheza na mshindi wa pili katika kundi lingine kitu ambacho ni faida kwao.

"Tunawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba ambao wanatupa sapoti popote pale tunapokwenda, iwe matokeo mazuri au mabaya, tuna kazi moja tu nchini Ivory Coast, ni kuwafurahisha," alisema kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >